JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA.

HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA

**AGENDA YA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI WA ROBO YA PILI YA MWAKA 2021/2022 WA TAREHE 03 -04/03/2022.**

**AJENDA NA. 02/03/2021/2022.**

**SIKU YA KWANZA;**

| | | |
|---|---|---|
| (i) | Dondoo Na. 13/03/2021/2022 | - Kufungua Mkutano. |
| (ii) | Dondoo Na. 14/03/2021/2022 | - Kuthibitisha Ajenda. |
| (iii) | Dondoo Na. 15/03/2021/2022 | - Kupokea taarifa kutoka kwa Wenyeviti wa Kamati za Maendeleo za Kata (WDC) Robo ya Pili 2021/2022. |
| (iv) | Dondoo Na16/03/2021/2022 | - Kuahirisha Mkutano. |

**SIKU YA PILI:**

| | | |
|---|---|---|
| (v) | Dondoo Na. 17/03/2021/2022 | - Maswali ya Papo kwa papo kwa Mwenyekiti na Mkurugenzi wa Halmashauri. |
| (vi) | Dondoo Na. 18/03/2021/2022 | - Kupokea taarifa kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji (W). |
| (Vii) | Dondoo Na. 20/03/2021/2022 | - Kusoma na kuthibitisha Muhtasari wa Mkutano wa Baraza la Madiwani wa tarehe **02-03/11/2021** |
| (viii) | Dondoo Na. 21/03/2021/2022 | - Kupokea taarifa kutoka kwa Wenyeviti wa Kamati za Kudumu.<br>(a) Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango<br>(b) Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira.<br>(c) Kamati ya Elimu na Afya .<br>(d) Kamati Shirikishi ya Kudhibiti UKIMWI.<br>(e) Kamati ya Maadili. |

(iX) Dondoo Na. 22/03/2021/2022- Kufunga Mkutano

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

## HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA

### MUHTASARI WA MKUTANO WA HALMASHAURI WA BARAZA LA MADIWANI KILICHOFANYIKA TAREHE 02 - 03/11/2021 KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI

### A: WAJUMBE WALIOHUDHURIA

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe.Thereza J.Lusangija | - Diwani Kata ya Ngudu | - Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Lucy C. Nchangwe | - Diwani V/Maalum | -M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Athanas Nigo | - Diwani Kata ya Malya | - Mjumbe |
| 4. | Mhe. Elias Kapunda | - Diwani Kata ya Walla | - Mjumbe |
| 5. | Mhe Peter Misalaba | - Diwani kata ya Nyambiti | - Mjumbe |
| 6. | Mhe. Majaliwa Mbasa | - Diwani Kata ya Ngulla | - Mjumbe |
| 7. | Mhe. Peter L. Ngassa | - Diwani Kata ya Nghundi | - Mjumbe |
| 8. | Mhe .Fati Samwel Mmbanda | - Diwani Kata ya Fukalo | - Mjumbe |
| 9. | Mhe. Philipo John Ndalahwa | - Diwani Kata ya Mwamala | - Mjumbe |
| 10. | Mhe. Bayega L. Nchimachalo | - Diwani Kata ya Bungulwa | - Mjumbe |
| 11. | Mhe. Debora M. Lameck | - Diwani Kata ya Mwakilyambiti | - Mjumbe |
| 12. | Mhe. Bukaba M. Masai | - Diwani Kata ya Hungumalwa | - Mjumbe |
| 13. | Mhe. Mapembe T. Ndododo | - Diwani Kata Maligisi | - Mjumbe |
| 14. | Mhe. Amosi Kiyuga | - Diwani Kata ya Ilula | - Mjumbe |
| 15. | Mhe. John Sababu | - Diwani Kata ya Mhande | - Mjumbe |
| 16. | Mhe.Sephania Cheyo | - Diwani Kata ya Bupamwa | - Mjumbe |
| 17. | Mhe. Amede S. Kijika | - Diwani Kata ya Mwabomba | - Mjumbe |
| 18. | Mhe. Joseph Katuli | - Diwani Kata ya Kikubiji | - Mjumbe |
| 19. | Mhe. Masanja M. Imaja | - Diwani Kata ya Igongwa | - Mjumbe |
| 20. | Mhe.Selemani L. Lutunduja | - Diwani Kata ya Lyoma | - Mjumbe |
| 21. | Mhe. Elias Galula | - Diwani Kata ya Shilembo | - Mjumbe |
| 22. | Mhe. Bukombe Nyanda | - Diwani Kata ya Nyamilama | - Mjumbe |
| 23. | Mhe. Gervas Kitwala | - Diwani Kata ya Sumve | - Mjumbe |
| 24. | Mhe. Hole L. Mashauri | - Diwani Kata ya Mantare | - Mjumbe |
| 25. | Mhe. Mayala Sagini | - Diwani Kata ya Mwandu | - Mjumbe |
| 26. | Mhe. Yohana S. Nyerere | - Diwani Kata ya Mwang'halanga | - Mjumbe |
| 27. | Mhe. Sanduli Malando | - Diwani Kata ya Mwankulwe | - Mjumbe |
| 28. | Mhe. Chenyenge John | - Diwani Kata ya Bugando | - Mjumbe |
| 29. | Mhe. Samson N. Masalu | - Diwani Kata ya Nkalalo | - Mjumbe |
| 30. | Mhe. Wenslaus Mapolu | - Diwani Kata ya Iseni | - Mjumbe |
| 31. | Mhe.Anthony Swagi | - Diwani Kata ya Mwagi | - Mjumbe |
| 32. | Mhe. Felista Joseph | - Diwani V/Maalum Sumve | - Mjumbe |
| 33. | Mhe. Veronica Manyongo | - Diwani Viti Maalum | - Mjumbe |
| 34. | Mhe. Devotha Manane | - Diwani V/Maalum Fukalo | Mjumbe |
| 35. | Mhe. Leah M. Joseph | - Diwani V/Maalum Nyamilama | - Mjumbe |
| 36. | Mhe. Teddy Alphonce | - Diwani V/Maalum | - Mjumbe |
| 37. | Mhe. Adellah Charles | - Diwani V/Maalumu | - Mjumbe |
| 38. | Mhe. Mamertha M. Kapaya | - Diwani V/Maalumu | - Mjumbe |
| 39. | Mhe. Winifrida P. Mahumbi | - Diwani V/Maalum | - Mjumbe |

40. Mhe. Khadija Ndode - Diwani Kata ya Ngudu - Mjumbe.
41. Mhe. Emmanuel K. Mageni (MB) - Jimbo la Sumve - Mjumbe
42. Ndg. Happiness J. Msanga - Mkurugenzi Mtendaji (W) - Katibu

**B. WAJUMBE AMBAO HAWAKUHUDHURIA KWA TAARIFA**

1. Mhe. Kabula E. Shitobela (MB) -V/Maalum Mkoa - Mjumbe
2. Mhe. Mansoor S. Hiran (MB) - Jimbo la Kwimba - Mjumbe

**C. WATAALAM WALIOHUDHURIA**

1. Ndg. Peter Revelian - Mweka Hazina (W)
2. Eng. Magreth Kavalo - Afisa Kilimo Umwagiliaji na Ushirika (W)
3. Ndg. Joshua Mgoli - Afisa Utumishi na Utawala (W)
4. Ndg. William Kasuja - Kaimu Afisa TEHAMA (W)
5. Ndg. Neema Joshua - Afisa Habari
6. Ndg. Kulwa John - Kaimu Afisa Manunuzi na Ugavi (W)
7. Ndg. Emmanuel Katemi - Afisa Elimu Sekondari (W)
8. Ndg. William Mbembela - Kaimu Afisa Maendeleo ya Jamii (W)
9. Ndg. Hamza H. Hamza - Afisa Tarafa Ngudu
10. Ndg. Kulwa Adrian - Kaimu Afisa Mtendaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo-Ngudu
11. Ndg. Nyamwiza Peter - Kaimu Afisa Elimu Msingi (W)
12. Ndg. Joseph Mambo - Kaimu Afisa Utamaduni (W)
13. Ndg. Godfrey Mwera - Kaimu Mganga Mkuu (W)
14. Ndg. NestoryMtewele - Kaimu Mkaguzi wa Ndani (W)
15. Ndg. Wickriph Benda - Afisa Ardhi na Maliasili (W)
16. Ndg. Serapion Rujuguru - Kaimu Afisa Mifugo na Uvuvi (W)
17. Ndg. Stephen B. Singira - Mwanasheria wa Halmashauri
18. Ndg. Edphonce Magwira - Kaimu Mhandisi wa Ujenzi na Zimamoto (W)
19. Ndg. Nesphory Biswalo - Afisa Usafi na Mazingira (W)
20. Ndg. Denis Kabogo - Afisa Uchaguzi
21. Ndg. Selestina Mushi - Mratibu wa TASAF
22. Ndg. Wivina Byabato - CHAC
23. Ndg. Greyson E. Vuri - Kaimu Afisa Nyuki (W)
24. Ndg. James Chuwa - Afisa Tarafa Ngula
25. Ndg. Patrick Michezo - Afisa Tarafa Ibindo
26. Ndg. Bonoventure Makungu - Kaimu Afisa Tarafa – Nyamilama
27. Ndg. Benedicto Seba - Kaimu Afisa Tarafa – Mwamashimba

**D.WAKARIBISHWA**

1. Mhe. Johari M. Samizi - Mkuu wa Wilaya
2. Ndg. Kamhamda Elia - Kaimu Kamishna Afisa Ardhi Mkoa
3. Ndg. Misana A. Bihemo - Afisa Mipango Miji Mkoa
4. Ndg. Frank M. Bihemo - Afisa Manunuzi Mkoa
5. Ndg. Oscar Tandula - IA - LGAs
6. Ndg. Elias Nyakia - Kaimu Katibu Tawala Msaidizi Serikali za Mitaa (M)
7. Ndg .Franciscar J. Mmari - PHRO
8. Ndg. Nyakia Ally - Katibu Tawala (W)
9. Ndg. Husein Muya - Kny. Katibu wa CCM (W)
10. Ndg. Musa Mkumba - Afisa Usalama (W)
11. ASP.V.P. Magessa - Mkuu wa Gereza (W)
12. ASP. M. Mayombo - Mkuu wa Polisi (W)
13. SP. Osward Mukuta - Afisa Uhamiaji

14. Capt.G.C.Mndeme - Mshauri wa Jeshi la Akiba
15. Ndg. Julian Augustine - Kamanda wa TAKUKURU
16. Eng. Dickson Lukanazya - Meneja TARURA
17. Ndg. Juma Said - Meneja MWAUWASA
18. Eng. Godliver Gwambasa - Meneja RUWASA
19. Ndg. Luciana Tito - Mratibu Afya ya jamii
20. Ndg. Amina Sufiani - Afisa Mradi AMREF
21. Ndg. Tawadu Yazid - Kaimu Meneja NMB
22. Ndg. Rehema Fungo - Kaimu meneja NIDA
23. Ndg. Richard Mganga - Mkuu wa Chuo cha Michezo Malya

**E. WAANDISHI WA HABARI**

1. Ndg. Gervas Mbaya - Mwandishi wa Habari TBC
2. Ndg. Henery Kavirondo - Mwandishi wa Habari CHANEL TEN

**F. SEKRETARIETI**

1. Ndg. Edmund M.Alois - Mwandishi wa Vikao
2. Ndg. Rahel A. Mdachi - Mwandishi wa Vikao
3. Ndg. Israel S. Petro - Mratibu wa Vikao

**KDC/F/C/AJENDA NA. 01/11/2021/2022 - AJENDA ZA MKUTANO**

**SIKU YA KWANZA**

1. Ajenda Na. 01/11/2021/2022 - Kufungua Mkutano
2. Ajenda Na. 02/11/2021/2022 - Kuthibitisha Ajenda
3. Ajenda Na. 03/11/2021/2022 - Taarifa za Taasisi
   - AMREF
   - RUWASA
   - TARURA
4. Ajenda Na. 04/11/2021/2022 - Kupokea taarifa kutoka kwa Wenyeviti wa Kamati za Maendeleo za Kata (WDC) za Robo ya I mwaka 2021/2022
5. Ajenda Na. 05/11/2021/2022 - Kuahirisha Mkutano

**<u>SIKU YA PILI:</u>**

6. Ajenda Na. 06/11/2021/2022 - Maswali ya Papo kwa papo kwa Mwenyekiti na Mkurugenzi wa Halmashauri.
7. Ajenda Na. 07/11/2021/2022 - Kupokea taarifa kutoka kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya.
8. Ajenda Na. 08/11/2021/2022 - Maelekezo kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa.
9. Ajenda Na. 09/11/2021/2022 - Kusoma na Kuthibitisha Muhtasari wa Mkutano wa Baraza la Madiwani wa tarehe 17-18/08/2021.
10. Ajenda Na.10/11/2021/2022 - Kupokea taarifa kutoka kwa Wenyeviti wa Kamati za Kudumu.
    - Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango
    - Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira
    - Kamati ya Elimu, Afya na Maji
    - Kamati Shirikishi ya Kuthibiti UKIMWI
    - Kamati ya Maadili

11. Ajenda Na.11/11/2021/2022 - Taarifa ya masuala ya Kiutumishi
12. Ajenda Na.12/11/2021/2022 - Kufunga Mkutano.

**SIKU YA KWANZA.**

**KDC/F/C/AJENDA NA. 01/11/2021/2022 - KUFUNGUA MKUTANO**
Katibu aliwaeleza Wajumbe hiki ni Kikao cha kwanza kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Akidi imetimia na alimkaribisha Mwenyekiti ambaye alifungua Kikao saa 3.50 Asubuhi.

**KDC/F/C/AJENDA NA. 02/11/2021/2022 – KUTHIBITISHA AJENDA**
Ajenda za Kikao zilithibitishwa na wajumbe.

**KDC/F/C/AJENDA NA. 03/11/2021/2022 – TAARIFA YA ASASI.**

- **Taarifa ya AMREF;**

Mratibu wa AMREF aliwasilisha taarifa juu ya mradi wa Ustawi wa Mwanamke unaohusisha Afya ya Uzazi na mtoto. Kupitia mradi huo wamefanikiwa kuajiri watoa huduma za Afya 10 na watawalipa mshahara kwa kipindi cha mwaka mmoja. Pia wametoa vitendea kazi mbalimbali kwa wahudumu wa Afya ngazi ya jamii. Pamoja na kutoa mafunzo ya kujikinga na ugonjwa wa UVIKO-19 kwa wahudumu wa Afya ngazi ya jamii na hasa umuhimu wa chanjo.

Baada ya Wajumbe kupokea taarifa hiyo walitaka kujua Wahudumu wataendelea kulipwa na Mradi kwa muda gani.

Wajumbe walijibiwa kwamba Mradi utawalipa Wahudumu 10 kwa muda mwaka mmoja

- **Taarifa ya RUWASA;**

Taarifa iliwasilishwa mbele ya Wajumbe na Meneja wa RUWASA akielezea utekelezaji wa miradi ya maji Vijijini mpango na vipaumbele vya miradi ya maji Vijijini.
Baada ya Wajumbe kupokea taarifa hiyo walipenda kujua miradi ya Maji iliyopitishwa kwenye Bajeti itaanza kutekelezwa lini na waliomba miradi ya maji izingatie uwiano wa Majimbo. Waliomba Shule zipelekewe miradi ya maji kwa sababu Serikali imejenga vyoo vya kisasa.

Wajumbe walipenda kujua utafiti wa maji chini ya Ardhi utaanza lini na waliomba maeneo yenye changamoto kubwa ya maji kama vile Shigangama Shilima na Kiliwi wapewe kipaumbele cha kwanza kupelekewa maji ya ziwa Victoria.

Meneja wa RUWASA alisema kuwa baadhi ya maeneo usanifu umefanyika kama Kijiji cha Sangu. Utafiti wa maji unafanywa na Makampuni ambayo yatahusika na uchimbaji wa visima 12.
Vilevile alieleza zoezi la kupima wingi wa maji linaendelea kwa baadhi ya Vijiji kama Isunga. Alieleza zoezi la kununua vifaa kwa ajili ya mradi wa Shilembo unaendelea. Aidha, alieleza Kijiji cha Shigangama kitawekwa kwenye Bajeti ijayo.

Aidha, Katibu Tawala Wilaya alisema mradi wa maji Shilima Mhe. Diwani akutane na Wataalamu ili kutatua changamoto zilizopo na alifafanua kuwa mradi wa maji Hungumalwa utasimamiwa na Serikali kuu.

- **Taarifa ya MWAUWASA;**

Taarifa iliwasilishwa na Meneja wa MWAUWASA ambapo alieleza mpango wa utekelezaji wa miradi ya maji, vipaumbele ,changamoto za mradi wa maji na mikakati ya kuboresha huduma za maji mjini.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kutaka kujua sababu za maji kukatika kwa muda mrefu na kusababisha ukosefu wa maji wakati Serikali imejenga Tanki kubwa kwa lengo la kuondoa adha ya maji kwa wateja katika Mji wa Ngudu na viunga vyake.

Meneja wa MWAUWASA alijibu kwamba changamoto imetokea baada ya bomba la maji kupasuka eneo la Lunele kwenda Mhalo kwa sababu mfumo wa miundo mbinu hiyo ni ya kizamani ilijengwa mwaka 1975. Utaratibu wa kubadili miundombinu hiyo inaendelea.

Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kuiridhia. Pia walishauri jitihada ziongezeke ili huduma ya maji irejee katika Mji wa Ngudu.

- **Taarifa ya TARURA;**

Meneja wa **TARURA** aliwasilisha taarifa ya utekelezaji shughuli za barabara, mpango wa utekelezaji changamoto mbalimbali na mikakati ya **TARURA.**

Baada ya Wajumbe kupokea taarifa hiyo waliomba baadhi ya Barabara zifunguliwe ili Wananchi waweze kupata huduma kutoka maeneo mengine. Baadhi ya Barabara hizo ni Barabara ya Kijida kwenda Nghuliku Barabara ya kutoka Lunele kwenda Kabale na Ibaya Shule ya Msingi, Barabara ya Nyamigamba – Iseni barabara ni mbovu itengenezwe Walieleza Maeneo ya Shilembo na Mwamitinje kuna Wakulima wengi wakubwa lakini hawana Barabara za kuwasaidia kusafirisha mazao yao, waliomba maeneo hayo yatengenezewe barabara ili wakulima waweze kusafirisha mazao yao .

Wajumbe walishauri Mkandarasi mmoja asipewe kutengeneza Barabara nyingi jambo linalosababisha kutomaliza kazi kwa wakati aliopangiwa. Walishauri wakandarasi wakaguliwe mara kwa mara kwasababu kuna baadhi ya wakandarasi hutengeneza chini ya kiwango ili iwasaidie kufanya marekebisho mapema.

Wajumbe waliomba baadhi ya maeneo yenye mito yajengewe madaraja ili kuwasaidia Wananchi na watoto kuvuka kwa usalama kama vile Kijiji cha Ndamhi kuna Shule ya Msingi wakati wa mvua watoto hushindwa kuvuka mto na baadhi ya watoto huzama wakati wa kuvuka wakienda shule. Pia walieleza Kata ya Bugando Wananchi wengi watoto wao husomea katika Sekondari ya Iseni ambako barabara ni mbovu pia wananchi mahitaji yao hupata kutoka Magu na kuna mto ambao ni hatari nyakati za masika.

Meneja wa TARURA alisema ushauri uliotolewa ameupokea, changamoto hawana usafiri na Watumishi ni wachache. Hata hivyo alisema baadhi ya maeneo taratibu za matengenezo zinaendelea. Barabara ya kwenda Iseni itawekwa kwenye Bajeti.

Alisema atatembelea eneo la Kijiji cha Ndamhi na Kata ya Bugando kuona namna ya kuweka kivuko. Pia alifafanua kwamba TARURA haitaweza kujenga daraja la Barabara ya Bugando kwenda Magu kwa vile upande wa pili ni mashamba hakuna Kaya.

Katibu Tawala wilaya alieleza kwamba kuhusu TARURA kupatiwa usafiri atalifikisha kwa Katibu Tawala Mkoa ili wapewe kipaumbele kwa magari yatakayo nunuliwa na Serikali.

Kuhusu uhaba wa Watumishi, alisema ni tatizo la nchi nzima, amelichukua atalifikisha kwa Katibu Tawala Mkoa.

Kuhusu ubora wa Barabara, alishauri watengeneze Barabara chache kwa ubora ili zidumu na kuisadia Jamii kwa kipindi kirefu.

Alishauri Shule Msingi Ndamhi iwekwe kwenye mpango wa Shule Shikizi ili watoto wa Kijiji cha Ndamhi wapate haki yao ya kupata elimu bila hofu ya kuzama kwenye mto nyakati za masika.

Kuhusu kuifungua Bugando alishauri Meneja wa TARURA akutane na Meneja wa TARURA Mkoa walijadili namna ya kufungua Bugando.

Wajumbe wa Baraza la Madiwani walishauri kwamba, Meneja wa TARURA akutane na Meneja wa TARURA Mkoa na Mkuu wa Wilaya wasaidie kuifungua Kata ya Bugando.

Wajumbe waliridhia mapendekezo yaliotolewa yawekwe kwenye utekelezaji

**Azimio Na. (01:11)**
Iliazimiwa na Wajumbe wa Baraza la Madiwani kwamba, Shule ya Msingi Ndamhi iwekewe Shule Shikizi ili kuwasaidia watoto wanaotoka maeneo ya mbali.

**Kuongeza siku 1 ya mkutano wa Baraza la Madiwani ili kuoitia taarifa za TARURA**

Mjumbe alitaka kujua kuhusu utekelezaji wa maelekezo ya Mhe.Rais Samia Suluhu Hassani kuwa Baraza la Madiwani kuwa na siku maalum ya kujadili masuala ya Barabara yanayosimamiwa na TARURA ili kuwa na uelewa wa pamoja

Meneja wa TARURA alijibu kuwa Bajeti ya kikao husika imeandaliwa na kutumwa Ofisi ya Rais –TAMISEMI kinachosubiriwa sasa ni maelekezo kwa ajili ya utekelezaji.

Wajumbe waliridhia mapendekezo yaliotolewa yawekwe kwenye utekelezaji

**KDC/F/C/AJENDA NA. 04/11/2021/2022 – KUPOKEA TAARIFA KUTOKA KWA WENYEVITI WA KAMATI ZA MAENDELEO WDC KWA KIPINDI CHA ROBO YA I JULAI – SEPTEMBA 2021/2022**

Taarifa za Wenyeviti wa Kamati kwa kipindi cha robo ya I Julai – Septemba ziliwasilishwa kwa Kata zote 30 na Wajumbe walizipokea.

**KDC/F/C/AJENDA NA. 05/11/2021/2022 – KUAHIRISHA KIKAO**

Mwenyekiti aliwashukuru Wajumbe kwa michango yao na aliahirisha kikao saa 10:40 jioni.

**SIKU YA PILI;**

- **Utambulisho;**

Mkurugenzi aliwatambulisha wageni kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa.

**KDC/F/C/AJENDA NA. 06/11/2021/2022 – MASWALI YA PAPO KWA PAPO**

- **Mapato ya Stendi ya mabasi Hungumalwa;**

Mjumbe alitaka kujua kiasi cha fedha kinachopatikana kabla na baada ya kufunga CCTV Kamera.

Mkurugenzi alijibu kwamba kabla ya kufunga CCTV Kamera Halmashauri ilikuwa ikikusanya Sh. 7,832,000.00 kwa mwezi na baada ya kufunga CCTV Kamera Halmashauri inakusanya Sh. 8,740,000.00 kwa mwezi.

- **Mali za Halmashauri;**

Mjumbe alitaka kujua taratibu zinazotakiwa ili Mwananchi aweze kutumia mali za Halmashauri.
Mkurugenzi alijibu kwamba utaratibu anaotakiwa mtu kuufuata anapotaka kutumia mali za Halmashauri ni kufuata Kanuni, Taratibu na Sheria.

- **Malipo ya Walinzi wa vizuizi;**

Mjumbe alitaka kujua sababu za Walinzi wa vizuizi kutolipwa kwa wakati malipo yao.
Mkurugenzi alijibu malipo ya Walinzi yanaendelea, na taratibu za malipo zikikamilika walinzi wanaodai watalipwa.

- **Wazabuni kucheleweshewa malipo;**

Mjumbe alitaka kujua sababu za Wakandarasi waliofanya kazi na Halmashauri kutolipwa kwa wakati.
Mkurugenzi Mtendaji alisema mfanyabiashara huingia Mkataba na Halmashauri. Hivyo, malipo yatazingatia Mkataba uliofungwa na kazi iliyofanyika kama imekamilika. Tatizo la mfumo wa malipo unaweza kuwa sababu ya kuchelewesha malipo pamoja na Mzabuni kutowasilisha vifaa kwa wakati .

**KDC/F/C/AJENDA NA. 07/11/2021/2022 – KUPOKEA TAARIFA KUTOKA KWA MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA**

Taarifa iliwasilishwa na Mkurugenzi mtendaji (W) ambapo alieleza kuwa katika Mwezi Oktoba 2021 Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba imepokea kiasi cha Tsh. 3,411,782,615.69 kwa ajili ya miradi mbalimbali kama ifuatavyo;

| | |
|---|---|
| • Ujenzi wa madarasa 109 Elimu Sekondari | Tzs 2,180,000,000.00 |
| • Ujenzi wa Kituo cha Afya kata ya Kikubiji | Tzs 250,000,000.00 |
| • Madeni ya Wazabuni na chakula mashuleni | Tzs 113,586,995.69 |
| • Mitihani Darasa la 4 | Tzs 243,996,120.00 |
| • Mitihani Darasa la 7 | Tzs 229,954,500.00 |
| • Mitihani Kidato cha 2 | Tzs 149,142,500.00 |
| • Mitihani Kidato cha 4 | Tzs 245,102,500.00 |

Pia alieleza kati ya fedha hizo kiasi cha Tsh. 2.180,000,000.00 ni kwa ajili ya madarasa 109 katika Shule za Sekondari 34 ambapo madarasa hayo yanatakiwa yakamilike ifikapo tarehe 15/12/2021 kulingana na maelekezo, ili wanafunzi wapate vyumba vya kusomea pindi shule zitakapofunguliwa mwaka 2022.

Aidha, Mkurugenzi Mtendaji Wilaya, aliwajulisha wajumbe kuwa Halmashauri imepokea fedha nyingine kiasi cha Tzs 75,000,000.00 zilizo tumwa katikati ya mwezi Septemba 2021 kwa ajili ya ukamilishaji wa Madarasa katika shule tatu (3) ambazo ni;
(I) Nyamigamba Sekondari Madarasa 2 kwa kiasi cha fedha Tzs 25,000,000.00
(II) Mwashilalage Sekondari Madarasa 2 kwa kiasi cha fedha Tzs 25,000,000.00 na
(III) Hungumalwa Sekondari Madarasa 2 kwa kiasi cha fedha Tzs 25,000,000.00

Vilevile alisema kuwa ununuzi wa vifaa utafanyika kwa pamoja 'bulk purchasing' ili kupunguza gharama na kurahisisha ufuatiliaji. Wajumbe walielezwa kuwa taratibu za kupata Wazabuni wa tofali zinaendelea na kazi zitafanywa kwa kutumia "Force Account" na BOQ zimeandaliwa kwa kufuata bei halisi ya vifaa

Aidha, walijulishwa kuwa kutakuwa na Kamati mbili za ufuatiliaji katika utekelezaji wa mradi huu ambazo ni Kamati ya Ufuatiliaji ya Mkoa na Kamati ya Ufuatiliaji ya Wilaya.

Kamati nyingine zitaundwa iwapo itaonekana kuwa zitarahisisha uendeshaji wa ndani katika utekelezaji wa mradi huu kama Kamati ya Ufuatiliaji ya Wilaya itaridhia na kuona umuhimu huo ili kuleta ufanisi na mikataba ya Wazabuni na mafundi itakuwepo kwa kila hatua ya mradi.

Baada ya Wajumbe kupitia taarifa hiyo waliipokea na kujadili kama ifuatavyo;-

Wajumbe walimpongeza Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuipatia Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba kiasi hicho kikubwa cha fedha kwa ajili ya ujenzi wa madarasa kwa Shule za Sekondari. Walishauri kuwa uwepo usimamizi mzuri katika matumizi ya fedha hizo na wah. Madiwani wajulishe kuhusu miradi inayotekelezwa katika maeneo yao.

Wajumbe walishauri walejee upya makadirio ya bei za michanga na kokoto kwa baadhi ya maeneo na kila eneo lipewe BOQ kulingana na gharama halisi za eneo, tofari zifyatuliwe katika eneo la mradi husika.

**Nasaha za Mkuu wa Wilaya**

Mhe. Johari Mussa Samizi Alizungumza kuhusu mambo yafuatayo:-

**Uongozi**
Alisema Kiongozi ni njia hivyo hapaswi kulalamika bali anapaswa kuonesha njia na ufumbuzi wa changamoto zinazojitokeza vilevile kusimamia shughuli za maendeleo ya wananchi zinazoendelea katika eneo lake kwa kuhamasisha umoja, mshikamano na ushirikiano.

**Fedha za UVIKO- 19**
Alisema sio jambo la kawaida kupata fedha za madarasa 119 kwa awamu moja, alisema kinachotakiwa ni kutekeleza na kusimamia madarasa hayo yakamilike. Pia Kamati za ufuatiliaji Kitaifa, Kimkoa, Kiwilaya na Kikata zimeundwa kwa ajili ya kuhakikisha mradi huo wa madarasa unakamilika kwa wakati.

Aidha, alisema Serikali imeendelea kuleta fedha nyingi ambapo imeleta fedha kiasi cha Tsh.300,000,000 kwaajili ya ujenzi wa chumba cha dharura katika Hospitali ya Wilaya, Kiasi cha Milioni 400,000,000.00 kwa ajili ya ununuzi wa mashine ya X-Ray kwenye Hospitali mpya ya Wilaya, Milioni 50,000,000.00 zitapelekwa Nkalalo kukamilisha madarasa, Kakora itapokea Milioni 100,000,000.00, Ukarabati wa Chuo cha Afya Ngudu kiasi cha shilingi miliono 100,000,000.00 zitapelekwa na Chuo cha Malya kimepelekewa fedha kiasi cha Milioni 400,000,000.00 na Kata ya Nkalalo itapelekewa Sh.150,000,000.00 za kukamilisha madarasa.

**Upangaji wa maeneo ya Machinga**
Alisema suala la kuwapanga machinga linaendelea kwa kuwapanga kwenye maeneo ambayo yamebainishwa kwani wapo maeneo ya pembezoni mwa barabara ambayo hayaruhusiwi Kisheria.

**RUWASA**
Alisema wamepokea fedha za UVIKO-19 kiasi cha shilingi Bilioni moja ambapo Jimbo la Kwimba lilipata shilingi Milioni 500,000,000.00 na Jimbo la Sumve lilipata shilingi Milioni 500,000,000.00 kwaajili ya kuboresha barabara.

**Sensa ya watu na makazi**
Alisema zoezi la Sensa ya watu na makazi litafanyika mwaka huu na Kamati zimeanza kuundwa ili kuweza kusaidia kukamilisha zoezi hilo ili Serikali ipate idadi kamili ya watu kwa ajili ya kuweza kupeleka huduma kwa wananchi. Alisisitiza uwepo ushirikiano ili shughuli zote hizo ziweze kufanikiwa.

**Upandaji wa miti.**

Alisema Kwimba inatakiwa kupanda miti ili kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa Nchini na kila Halmashauri inatakiwa kupanda miti Milioni moja kwa mwaka, aliomba uhamasishaji ufanyike ili wananchi wapande miti katika maeneo yao.

Baada ya taarifa hiyo alimtambulisha Mkuu wa Afisa Usalama wa Taifa (W) Ndg. Mussa Shaban Mkumba ambaye aliomba ushirikiano katika usimamizi na utekelezaji wa shughuli mbalimbali ikiwemo miradi ya maendeleo.

**KDC/F/C/AJENDA NA. 08/11/2021/2022 – MAELEKEZO KUTOKA OFISI YA MKUU WA MKOA**

**Masuala ya Ardhi.**

Kamishina wa Aridhi Msaidizi Mkoa aliwaleza wajumbe kwamba Ardhi ni mali ya Serikali , Ardhi inatakiwa ipangwe kwa matumizi mbalimbali. Alieleza Ardhi ina mifumo miwili ya usimamizi ambayo ni usimamizi ngazi ya Kijiji na usimamizi ngazi ya Halmashauri, aliendelea kueleza kuwa sheria inaelekeza kutenga maeneo ya huduma za jamii kwa kushirikisha wananchi.Pia alieleza kuna sheria ya utoaji wa Ardhi kwa manufaa ya Umma. Vilevile alieleza kuwa Waheshimiwa madiwani watambue kwamba wananafasi kubwa katika usimamizi na upangaji wa Ardhi.

Kuhusu migogoro ya ardhi alisema kunamigogoro mingi ya Ardhi katika jamii ambayo inatakiwa itatuliwe kwenye Mabaraza ya Ardhi ambapo Baraza la Ardhi limeanzishwa na kutangazwa kwenye gazeti la Serikali.
Kuhusu ulipaji wa kodi ya Ardhi, aliwaomba waheshimiwa Madiwani wahamasishe wananchi kulipa kodi ya Ardhi kwani kutokufanya hivyo atakabiliwa na mkondo wa sheria.

**Utawala Bora**

Afisa Utumishi Mwandamizi Mkoa, alitoa ufafanuzi kuhusu mgongano wa Maslahi na alieleza athari zake ikiwemo kufifisha maamuzi,kupoteza imani kwa wananchi,kusababisha kupoteza haki ya anayestahili.
**Njia ya kuondoa mgongano wa maslahi** ni pamoja na kusimamia kanuni, taratibu, sheria, na kujitoa kwenye maamuzi kama unamaslahi pamoja na kutoa taarifa kwa uwazi.

**Afisa Manunuzi wa Mkoa**

Aliwaeleza wajumbe kuhusu taratibu za manunuzi kwamba aliyepewa mamlaka ya ununuzi ni mkurugenzi mtendaji kupitia kitengo cha manunuzi na kama itampendeza anaweza kukasimu madaraka kwenye taasisi ngazi za chini.
Misingi ya ununuzi ni uwazi, uwajibikaji,Utaalamu, Uadilifu, kuzingatia thamani ya fedha, kupata mzabuni au mtoa huduma sahihi, kuzingatia muda sahihi wa makubaliano, kiasi cha fedha sahihi na BOQ ziandaliwe kwa usahihi kulingana na bei halisi.

**KDC/F/C/AJENDA NA. 09/11/2021/2022 – KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI WA TAREHE 17-18/08/2021**

Muhtasari ulisomwa na Ukathibitishwa na Wajumbe wa Mkutano.

**KDC/F/C/AJENDA NA. 10/11/2021/2022 – KUPOKEA TAARIFA KUTOKA KWA WENYEVITI WA KAMATI.**

- **Kamati ya Fedha**

Mwakilishi wa Mwenyekiti wa kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango aliwasilisha taarifa ya kazi zilizofanywa na Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kwa kipindi cha robo ya I Julai –

Septemba 2021 na kutoa mapendekezo yao ambao yalipokelewa na Baraza kuwa kumbukumbu sahihi za Halmashauri, ambapo Kamati ilipendekeza Menejimenti ifuatilie na kuchukua hatua ya kuwaondoa waliovamia na kujenga nyumba eneo la Mnada wa Bungulwa pamoja na kuhakikisha maeneo mengine ya Ardhi ya Halmashauri hayavamiwi na Wananchi

Kamati ilitoa mapendekezo Kwamba, Jengo jipya la makao makuu ya Halmashauri linalotarajiwa kujengwa katika bajeti ya Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2021/2022 lijengwe katika eneo la Kitongoji cha Ilamba.
Vilevile, jengo la ofisi za mradi wa umwagiliaji Kimiza lisitumike kwa shughuli za zahanati ya kijiji cha Kimiza.

Wajumbe walipokea na kuipitisha kuwa kumbukumbu bila hoja.

**Kamati ya Uchumi Ujenzi na Mazingira**

Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira aliwasilisha taarifa ya shughuli zilizofanywa na Kamati kwa kipindi cha robo ya I Julai – Septemba 2021. Kamati ilipendekeza Idara ya Mazingira iendelee kutoa elimu ya upandaji miti hasa ya matunda kwa vikundi mbalimbali kwenye vyanzo vya maji na Taasisi za Serikali.

Kamati ilipendekeza elimu ya uboreshaji mazingira ya ufugaji nyuki itolewe kwa jamii ili wananchi waweze kuinua uchumi kwa kuuza mazao yatokanayo na ufugaji wa nyuki (Asali) ,Kamati ilipendekeza Idara ya Mifugo ifanye usafi wa mara kwa mara kwenye machinjio na bucha za nyama, Kamati ilipendekeza tathmini ifanyike ili kujua gharama za ukamilishaji jengo la Kantini, Kamati ilipendekeza maeneo ya Shule yenye migogoro yapimwe ili waweze kuitambua mipaka ya Shule na kuondoa migogoro kati ya Shule na Jamii.

Vilevile kamati ilipendekeza kwamba taarifa ya ukaguzi wa ukarabati wa ukumbi na Ofisi ya Mkurugenzi ipelekwe Baraza pia kamati ilipendekeza kwamba, Menejimenti itoe ufafanuzi wa majukumu ya Kamati ya Uchumi na Kamati ya Elimu katika ukaguzi wa miundombinu ya majengo.
Wajumbe walipokea mapendekezo matatu kuwa kumbukumbu, walishauri mapendekezo mengine yakajadiliwe kwenye Vikao vya Kamati
Wajumbe walipokea na kuipitisha kuwa kumbukumbu bila hoja.

- **Kamati ya Elimu na Afya**

Mwenyekiti wa Kamati ya Elimu na Afya aliwasilisha taarifa ambapo alieleza kuwa kamati ilipitia shughuli zilizofanywa na idara mbalimbali katika kipindi cha robo ya I Julai – Septemba 2021/2022 kisha Kamati ilipendekeza kwamba Mhandisi wa Ujenzi awashirikishe mafundi wazoefu katika kukadiria vifaa vya ujenzi. Aidha, Mhandisi atakayefanya makadirio ya vifaa vya ujenzi vikapungua au kuzidi atawajibika, Kamati ilipendekeza kwamba, meneja wa TARURA aje kwenye baraza kutoa ufafanuzi wa ujenzi huo.

Kamati ilipendekeza kwamba, Shule ya Sekondari Maligisu ijengewe uzio unaotenganisha Shule na nyumba ya kulala wageni, Kamati ilipendekeza kwamba, taarifa ya Kata zilizopewa fedha za mapato ya ndani ipelekwe kwenye Kamati ya fedha, Kamati ilipendekeza kwamba, kila Mheshimiwa Diwani asimamie Shule ambazo hazijatumia mbao zilizotolewa na Halmashauri zirejeshwe Halmashauri ili

zipewe Shule zenye uhitaji. Kamati ilipendekeza kwamba, kila Diwani asimamie matumizi ya fedha za ukarabati kwenye Shule zake na Kamati ilipendekeza kwamba, milango ya Kituo cha Afya Kadashi ifungwe, Vilevile kamati ilipendekeza kwamba, ufuatiliaji ufanyike wa gharama ya ununuzi wa betri ya sola katika Zahanati ya Kiliwi.

**Kamati ya Maadili.**

Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Kamati yake kwa kupindi cha robo ya I Julai – Septemba 2021/2022. Alieleza kuwa katika kikao Kamati ilipendekeza na kusisitiza wajumbe wazingatie kuwahi muda wa kuanza vikao vya kamati na Baraza ambao ni saa 4.00 asubuhi , Pia kamati ilipendekeza kila Mhe. Diwani asome vipengele vya Kanuni za Maadili wazielewe vizuri na sehemu ambazo zinahitaji ufafanuzi ziwasilishwe kwenye kamati ya Maadili kwaajili ya ufafanuzi zaidi.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kushauri Waheshimiwa Madiwani wasome na kuzielewa Kanuni za Maadili za Madiwani.

**Kamati Shirikishi ya kudhibiti UKUMWI**

Taarifa ilisomwa na mjumbe wa kamati kwaniaba ya Mwenyeki alieleza kuwa katika kipindi cha robo ya kwanza 2021/2022 kamati ilipitia shughuli mbalimbali zilizofanyika za mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU na ilitoa mapendekezo yafuatayo; kamati ilipendekeza katika bajeti ya mwaka 2022/2023 itengwe bajeti ya kununua vitendea kazi ikiwemo usafiri pia Kamati ilipendekeza elimu juu ya athari za ugonjwa wa UKIMWI na mbinu za kujikinga ili jamii iamini kuwa ugonjwa upo iachane na mila potofu za kulogwa.

Aidha Kamati ilipendekeza wawakilishi wa makundi mbalimbali yanayojihusisha na mapambano dhidi ya UKIMWI Ngazi ya Jamii wasome taarifa ya shughuli wanazozifanya kwenye vikao vya maendeleo ya Kata na Kamati ilipendekeza elimu iendelee kutolewa kuhusu matumizi sahihi ya Kondomu. Wajumbe walipokea taarifa na mapendekezo yake na kushauri Kondomu ziwekwe maeneo mbalimbali ili Wananchi waweze kuzipata kwa urahisi.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kuiridhia

**KDC/F/C/AJENDA NA. 11/11/2021/2022 – TAARIFA YA MASUALA YA WATUMISHI DHIDI YA ALIYEKUWA MSIMAMIZI WA MRADI WA VYOO VYA WASH.**

Baraza lilijigeuza kama Kamati ili kujadili na kutoa maamuzi.

**KDC/F/C/AJENDA NA. 12/11/2021/2022 – KUFUNGA MKUTANO**

Katibu aliwashukuru Wajumbe kwa michango yao kisha alimkaribisha Mwenyekiti ambaye alifunga Kikao saa 2:30 Usiku.

**UMETHIBITISHWA.**

| ................................ | ...................................... | .................................. |
|---|---|---|
| MWENYEKITI | TAREHE | KATIBU |

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA**

**Mhe. Mwenyekiti**,
Baraza la Madiwani
**HALMASHAURI YA KWIMBA.**

**YAH: TAARIFA YA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO ROBO YA PILI - MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

Mhe,Mwenyekiti naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Fedha Uongozi na Mipango kwa kipindi cha robo ya pili kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kama ifuatavyo;

**WAJUMBE WA KAMATI:**
Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango ina jumla ya Wajumbe kumi na mbili na majina ya wajumbe ni kama ifuatavyo hapa chini;-

| | | |
|---|---|---|
| 1. Mhe. Thereza J. Lusangija | - Diwani Kata ya Ngudu | - Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Lucy Nchangwe | - Diwani Viti Maalum | - M/M/kiti |
| 3. Mhe. Debora L. Mapembe | - Diwani Kata ya Mwakilyambiti | - Mjumbe |
| 4. Mhe. Peter M. Nyanda | - Diwani Kata ya Nyambiti | - Mjumbe |
| 5. Mhe. Elias M. Kapunda | - Diwani Kata ya Walla | - Mjumbe |
| 6. Mhe. Seleman L. Lutunduja | - Diwani Kata ya Lyoma | - Mjumbe |
| 7. Mhe. Amos Kiyuga | - Diwani Kata ya Ilula | - Mjumbe |
| 8. Mhe. Fati S. Mmbanda | - Diwani Kata ya Fukalo | - Mjumbe |
| 9. Mhe. Mamertha M. Kapaya | - Diwani Viti Maalum | - Mjumbe |
| 10.Mhe. Felister L. Joseph | - Diwani Viti Maalum | - Mjumbe |
| 11.Mhe. Kasalali E. Mageni(Mb) | - Jimbo la Sumve | - Mjumbe |
| 12.Mhe. Mansoor S. Hiran (Mb) | - Jimbo la Kwimba | - Mjumbe |

Mkurugenzi Mtendaji (W) ndiye Katibu wa Kamati, na Wakuu wote wa Idara na Vitengo pia wanawajibika kwa mujibu wa Sheria kuhudhuria na kushiriki katika vikao vya Kamati hii.

**VIKAO VYA KAMATI:**
**Mhe. Mwenyekiti,**
Katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka wa fedha 2021/2022 Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango imefanya jumla ya vikao vitatu vya kawaida . Kwa muhtasari, kupitia vikao hivyo, Kamati iliweza kusimamia makusanyo ya mapato na matumizi ya fedha za Halmashauri, kupitia na kujadili taarifa ya Mapokezi ya Fedha za miradi ya maendeleo kiasi cha sh 3,411,782,615.69,kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 109 Elimu Sekondari sh 2,180,000,000.00 Ujenzi wa kituo cha Afya sh250.000.000.00 madeni ya wazabuni sh 113,586,995.69 mitihani ya darasa la nne sh 243,996120.00 ,mtihani wa darasa la saba sh 229,954,500,kidato cha pili sh 149,142,500.00na kidato cha nne . sh 245,102,500.00 kupitia taarifa ya mkaguzi wa ndani robo ya I mwaka 2021/2022 kuidhinisha mapendekezo ya kutumia vifungu vingine kulipa wakusanya mapato kuidhinisha msawazisho wa vifungu. Kamati iliweza kuidinisha maombi ya kubadili matumizi ya

fedha za RBF sh 450,000,000.00. kamati iliidhinisha mapendkezo ya kutoa mikopo ya vikundi vya wanawake vijana na watu wenye ulemavu kiasi cha sh 120,000,000.00 . Kamati pia ilipitia taarifa ya michezo ya kubahatisha pamoja na maeneo ya wafanyabiashara wadogo (wamachinga ), kupitia na kujadili taarifa ya Utendaji wa Halmashauri katika kipindi cha robo mwaka husika, na kupitia taarifa ya miradi itakayotekelezwa na TASAF, Vilevile Kamati iliweza kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Utoaji wa huduma za Afya na mfumo wa Ukusanyaji mapato katika kituo cha Afya Nyamilama ujenzi wa madarasa 2 katika Shule ya Sekondari Nyamilama pamoja na miundo mbinu ya kutolea huduma katika Shule ya Msingi Kabale. Majukumu haya yote yametekelezwa na Kamati chini ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Kanuni za Kudumu za Halmashauri, Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 na Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 pamoja na Kanuni zake.

## TAARIFA YA KINA YA KAZI ZILIZOTEKELEZWA NA HALMASHAURI CHINI YA USIMAMIZI WA KAMATI:

Katika kipindi cha robo ya pili ya Mwaka 2021/2022 Kamati ilisimamia utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya Halmashauri katika sekta za Fedha, Utumishi na Utawala, Sheria, Manunuzi, Mipango,Takwimu na Ufuatiliaji, na TEHAMA kama taarifa ya utendaji wa shughuli hizo inavyoonekana hapa chini;-

### 1: Hali ya kifedha ya Halmashauri:

**Mhe Mwenyekiti,**

**MAPATO/MAPOKEZI YA FEDHA**

Kwa mwaka wa Fedha 2021/2022 Halmashauri iliidhinishiwa kukusanya, kupokea na kutumia jumla ya Sh. 56,222,895,102.80 na nyongeza ya bajeti sh 2,962,076,434.35 iliyotokana na nyongeza ya matumizi mengineyo sh 113,586,995.69 na kwenye miradi ya maendeleo sh 2,848,489,438.66 hivyo kufanya jumla ya bajeti ya mwaka 2021/2022 kuwa sh 59,184,971,537.15 kutoka katika vyanzo mbalimbali

**Mapato ya Ndani**:

Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba iliidhinishiwa kukusanya jumla ya **Sh. 2,467,985,000.00** ikiwa ni mapato ya ndani. Kati ya makisio hayo sh 841,144.000.00 ni mapato lindwa na sh 1,626,841,000.00 ni mapato yasiyolindwa. Kwa mwezi Desemba 2022 Halmashauri ilikusanya **Sh 111,079,910.88** kati ya mapato hayo sh 27,551,896.48 ni mapato lindwa na sh 83.528,014.40 ni mapato yasiyolindwa. Hivyo basi kuanzia Julai 2021 hadi kufikia mwezi Desemba 2021 Halmashauri ilikuwa imekusanya kiasi cha **sh. 1,298,404,835.70** sawa na 52.61% ya lengo la makusanyo ya ndani Aidha kwa mwaka wa fedha 2020/21Halmashauri iliidhinishiwa kukusanya **Sh. 2,353,488,200.00** hivyo basi kuanzia 01 Julai 2020 hadi Desemba 2021 Halmashauri ilikuwa imekusanya kiasi cha **Sh. 1,319,291,144.01** sawa na asilimia 56.06 ya bajeti ya mwaka husika..

Licha ya mafanikio ya ukusanyaji kama ilivyoelezwa, Kamati ya Fedha kwa upande wake kupitia vikao vyake imeendelea kusisitiza menejiminti kuongeza jitihada katika usimamizi ikiwemo uwekaji wa vizuizi vya barabarani na ulipaji wa posho za wakusanya mapato na kuchukua hatua za kiutawala au kinidhamu kwa watumishi wanaohujumu shughuli za ukusanyaji wa mapato hasa wale ambao hawawasilishi makusanyo ya mapato benki kwa wakati.

**Mishahara**:
Halmashauri iliidhinishiwa kupokea kiasi cha **Sh. 35,680,946,843.00** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 hadi kufikia Desemba 2021 Halmashauri ilikuwa imepokea jumla ya **Sh.15,348,459,000** sawa na asilimia 43.02 ya lengo la mapokezi ya fedha za mishahara kwa mwaka.
**Matumizi mengineyo (OC)**:
Halmashauri ilikisia kupokea jumla ya **Sh. 2,597,180,949.80** kwa ajili ya matumizi mengineyo na nyongeza ya bajeti **Sh 113,586,995.69** hivyo kufanya jumla ya bajeti ya mwaka 2021/2022 kuwa **Sh. 2,710,767,945.49**. Hadi kufikia mwezi Desemba 2021 Halmashauri ilikuwa imepokea jumla ya **Sh.680,331,766.86** sawa na asilimia **25.10** ya lengo la mapokezi ya fedha kwa mwaka mzima.

**Miradi ya Maendeleo**
Kwa upande wa miradi ya Maendeleo, kwa mwaka 2021/22 Halmashauri ilikisia kupokea na kutumia jumla ya **Sh.15,476,782,310** na nyongeza ya bajeti **Sh 2,848,489,438.66** hivyo kufanya jumla ya bajeti ya mwaka 2021/2022 kuwa **Sh. 18,325,271,748.66** hadi kufikia mwezi Desemba 2021 Halmashauri ilikuwa imepokea kiasi cha **Sh. 11,008,858,706.21** ikiwa ni sawa na **60.07** ya lengo la mwaka mzima.

Aidha, kutoka katika makusanyo ya mapato yake ya ndani kwa kipindi husika Halmashauri ilikisia kupeleka jumla ya **Sh.650,736,400** katika uchangiaji wa miradi ya maendeleo. Hadi robo ya pili ya mwaka inamalizika Halmashauri imeweza kupeleka **Sh. 106,874,880.00** sawa na asilimia **16.42**

**MATUMIZI:**
Katika mwaka wa fedha 2021/22 Halmashauri iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Sh. 56,222,895,102.80 na nyongeza ya bajeti sh 2,962,076,434.35 iliyotokana na nyongeza ya matumizi mengineyo sh 113,586,995.69 na kwenye miradi ya maendeleo sh 2,848,489,438.66 hivyo kufanya jumla ya bajeti ya mwaka 2021/2022 kuwa sh 59,184,971,537.17** kutoka katika vyanzo mbalimbali vya mapato. Hata hivyo, hadi kufikia Desemba 2021 Halmashauri iliweza kutumia jumla ya **Sh. 21,880,283,617.51** sawa na 36.97% ya lengo la mwaka ambapo kati ya fedha hizo, **Sh.915,980,118.82** ilikuwa ni mapato ya ndani, **Sh 433,882,295.69** ilikuwa ni Ruzuku ya matumizi mengineyo, **Sh. 15,348,459,000.00** ilikuwa ni mishahara na **Sh.5,182,262,203.00** ilikuwa ni miradi ya maendeleo.

<u>**2: Utumishi na Utawala:**</u>

<u>**Mh. Mwenyekiti**</u>
Kamati ya Fedha Uongozi na Mipango pia inasimamia masuala yanayohusu utawala na Utumishi katika ngazi zote za Halmashauri. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa vikao vya kisheria katika ngazi ya Halmashauri, Kata na Vijiji vinafanyika. Katika kipindi cha robo mwaka iliyomalizika mwezi Desemba 2021 vikao vyote vya Kamati za kudumu za Halmashauri vilifanyika. Aidha vikao vya Serikali za Vijiji vilivyofanyika ni 203, mikutano mikuu ni 84 na vikao vya Kamati za Kata ni 27 .

Pia, katika kipindi cha robo mwaka iliyomalizika, Kamati ilipokea na kupitia taarifa juu ya hali ya watumishi katika Halmashauri. Kumbukumbu zinaonyesha kuwa hadi kufikia mwezi Desemba 2021 Halmashauri ilikuwa na jumla ya watumishi 3,103 waliolipwa mishahara yao kupitia Hazina.
Kwa upande mwingine katika kipindi cha robo mwaka iliyomalizika Kamati ilipokea taarifa ya usafishaji wa taarifa za watumishi kwenye mifumo ambapo taarifa za watumishi 80 zilirekebishwa kwenye mfumo. Kamati ilipokea taarifa ya usimamizi wa utendaji kazi wa watumishi wanaofanya kazi ngazi ya Wilaya Kata na Vijiji . kamati ilipokea taarifa ya shughuli za ruhusa mbalimbali zilizotolewa , Shughuri za mlalamiko ya watumishi na wanachi.,kushughulikia madai ya watumishi na wastaafu kwenye mfuko wa hifadhi ya jamii
<u>**3: Masuala ya Kisheria:**</u>

**Mh. Mwenyekiti**
Katika kipindi cha robo mwaka iliyopita Kamati iliweza kujulishwa kuwa Halmashauri ilikuwa na jumla ya mashauri 7 ambayo yapo katika Mahakama mbalimbali. Aidha, kuna mashauri mengine 3 ambayo yapo kwenye hatua ya kusikilizwaji na mashauri manne yapo kwenye hatua za utekelezaji wa hukumu, na Halmashauri ndio inawajibika kuwalipa wadai husika. Majina ya mashauri yanayoendelea, wahusika pamoja na mahakama ambazo mashauri hayo yanaendeshwa ni kama inavyoonekana :

- Shauri la Ardhi Na. 259/2011 Isaya Daud Ngh'uguku dhidi ya Sebastian Kuyomba na Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba (Lipo Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Mwanza katika hatua ya usikilizwaji).
- Shauri la ardhi Na. 27 la mwaka 2021 Mponeja Manyilizu msimamizi wa mirathi ya Manyilizu Mponeja Mpangalala dhidi ya Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba (Lipo katika hatua ya awali madai yameshawasilishwa Mahakamani
- Shauri la ardhi Na.12/2021 Jinanai Duka dhidi ya Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba, Halashauri ya Kijiji cha Bupamwa, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wengine 19 ( Lipo Mahakama Kuu Mwanza katika hatua za awali za usikilizwaji.)

**4: Miradi ya maendeleo:**

**Mh. Mwenyekiti**

Kwa mwaka 2021/22 Halmashauri ilikisia kupokea na kutumia jumla ya **Sh.15,476,782,310**. Na nyongeza ya miradi ya maendeleo ambayo ni sh **2,848,489,438.66** na kufikia sh **18,325,271,748.66** hadi kufikia mwezi Desemba 2021 Halmashauri ilikuwa imepokea kiasi cha **Sh. 11,285,524,371.32** kutoka Serikali Kuu ikiwa ni sawa na **72.92%** ya lengo la mwaka mzima.
Aidha, kutoka katika makusanyo ya mapato yake ya ndani kwa kipindi husika Halmashauri ilikisia kupeleka jumla ya **Sh.650,736,400.00** katika uchangiaji wa miradi ya maendeleo ambapo hadi robo ya kwanza ya mwaka inamalizika Halmashauri imeweza kupeleka **Sh. 339,886,497.42** sawa na asilimia **52.23.** Kati ya fedha hizo **Sh. 96,121,599.36** ni za mfuko wa wanawake, vijana na wenye ulemavu na **Sh. 243,764,898.06** ni za miradi ya maendeleo.

Kamati pia iliweza kupata fursa ya kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Miradi hiyo ni; eneo linalokusudiwa kujengwa jengo la makao makuu ya Halmashauri ( Kitongoji cha Ilamba), ukamilishaji wa darasa moja Shule ya Msingi Kinamweli, ujenzi wa zahanati shule ya Msingi Nkungulu, ukamilishaji wa zahanati kijiji cha Busule, ukamilishaji wa chumba cha maabara shule ya Sekondari Mwankulwe, ujenzi wa barabara ya Ngogo – Mhulula (TARURA), ujenzi wa daraja barabara ya Isagala – Walla – Bungulwa (TARURA), mradi wa mashine ya kusagisha nafaka (Kikundi cha Maisha –Runele) na ujenzi wa matundu 12 ya vyoo katika shule ya Msingi ilebelo. Kamati iliweza kukagua miradi husika na kutoa ushauri katika maeneo mbalimbali kwa Menejimenti ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa miradi hiyo.

**5: Ukaguzi wa hesabu za Halmashauri.**
**Mhe. Mwenyekiti**
Katika kipindi cha robo mwaka iliyomalizika Kamati ilipata fursa ya kupitia taarifa ya Mkaguzi wa ndani ya robo ya I ya mwaka wa fedha 2021/2022. Taarifa hiyo ilibainisha uwepo wa jumla ya hoja za ukaguzi 20 ambapo hoja Moja iliweza kujibiwa kikamilifu na hoja 19 zipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Kutokana na hali ya utekelezaji wa hoja kutokuwa ya kuridhisha Kamati iliagiza

Menejimenti ijibu hoja za mkaguzi wa ndani kwa haraka na kuchukua hatua kwa wahusika walioshindwa kujibu hajo kwa wakati.

**6: Manunuzi:**

**Mhe. Mwenyekiti**

Katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2021/2022 iliyomalizika Halmashauri iliweza kufanya manunuzi mbalimbali kupitia Kitengo cha Ugavi. Manunuzi hayo ni pamoja na manunuzi ya huduma mbalimbali yenye thamani ya **Sh.127,506,995.69** na manunuzi ya vifaa mbalimbali vyenye thamani ya **Tsh 266,134,203.23** na kufanya jumla kuu ya manunuzi yote kuwa **Tsh.393,641,198.92**

**7: TEHAMA**

**Mhe. Mwenyekiti,**

Katika kipindi cha robo mwaka iliyomalizika Kamati iliweza kupitia taarifa ya Kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano na kuweza kujulishwa kuwa Kitengo cha TEHAMA kimeweza kushughulikia na kuhakikisha kuwa mifumo ya kielektroniki ya mapato na matumizi, mishahara na kiutumishi, na wavuti ya Halmashari vinafanya kazi kwa ufasaha.

Aidha, Kamati ilitaarifiwa kuwa shughuli nyingine zilizofanyika katika Kitengo hiki zilikuwa ni pamoja na kutoa msaada wa kiufundi na kitaalamu kwa watumiaji wa vifaa na mifumo ya TEHAMA na utengenezaji wa printa na POS zilizoharibika. Attendence Biometric Register . kushiriki katika kuandaa na kutoa habari kwa wananchi kupitia tovuti ya Halmashauri na mitandao ya kijamii.

**8: UCHAGUZI**

**Mhe. Mwenyekiti**

Katika kipindi cha robo mwaka iliyomalizika shughuli kuu iliyofanyika katika Sekta ya Uchaguzi ilikuwa ni kufuata vifaa vilivyobaki wakati wa uchaguzi wa Serkali za Mitaa kwa mwaka 2019 Kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa miradi mbalimbali iliwepo miradi ya UVIKO 19 na ujenzi wa kituo cha Afya Bungulwa.

Kushiriki katika kukusanya mapato ya Halmashauri kupitia doria za usiku .

**9; MJI MDOGO**

**Mhe, mwenyekiti**

Kamati ilipitia taarifa ya Mji mdogo wa Ngudu ambapo katika kipindi cha robo mwaka husika shughuri zilizofanyika ni kufanya ukaguzi na ufuatiliaji wa miradi UVIKO 19 Ngudu na Bujiku Sekondari,Ujenzi wa shule mpya ya Kilyaboya.

Kutembelea maeneo ya Serikali yaliyovamiwa na wananchi katika msitu wa Mwamakelemo ambapo kuna chanzo cha maji katika lambo la magiligita Bugakama na kufanya kikao na wananchi 12 waliovamia na kufanya shughuli za kilimo.

Kuwapanga wafanyabiashara wadogo katika maeneo rasmi yaliyoainishwa katika soko jipya na maeneo ya NIDA jumla ya wafanyabiashara 440 wamepangiwa maeneo. Pamoja na kusimamia ukusanyaji wa mapato katika Mji wa Ngudu.

Aidha, kamati yako imepitisha maombi ya utekelezaji wa miradi ya TASAF.inayotekelezwa kisekta katika utoaji huduma za Elimu Msingi na Sekondari pamoja na Afya.Miradi ya kutoa ajira kwa muda ( PWP= Public Works Program) na miradi ya kuongeza kipato( income generating Activity) IGA

**MAPENDEKEZO YA KAMATI:**

**Mhe. Mwenyekiti**
Pamoja na maombi ya kuridhiwa kwa taarifa hii kuwa kumbukumbu sahihi ya Halmashuri, Kamati inaomba kuwasilisha mapendekezo mengine yafuatayo ili kuweza kuridhiwa na kuwa maazimio ya Baraza:-

(i) Kamati ilipendekeza kwamba watendaji wanaodai stahiki zao za uhamisho walipwe.

(ii) Kamati ilipendekeza Kwamba wafanyabiashara wadogowadogo wahamishiwe kwenye maeneo yaliopangwa.

(iii) Kamati ilipendekeza kwamba Menejimenti ifuatilie maeneo yaliyofungwa mashine za michezo ya kubahatisha ili wazingatie muda wanaopaswa kucheza pamoja na kutoruhusu watoto na wanafunzi kushiriki mchezo huo.

(iv) Kamati ilipendekeza kwamba Menejimenti ifuatilie ifuatilie TANROAD na TARURA ili wakandarasi walioacha mashimo kandokando ya barabara yaweze kufukiwa kwavile ni hatari kwa watumiaji wa barabara, jamii na watoto pindi yanapojaa maji.

(v) Kamati ilipendekeza maeneo ambayo magari hutumia katika kutorosha mazao yawekewe vizuizi.

(vi) Kamati iliridhia maombi ya utekelezaji miradi ya TASAF na ikapendekeza katika mgawanyo wa miradi ya TASAF na miradi mingine itakayoletwa izingatie uwiano wa majimbo.

(Vii) Kamati ilipendekeza Kwamba wajumbe wa mabaraza ya ardhi wapewe semina juu ya utekelezaji wa majukumu yao kwani wanawaumiza wananchi katika kutatua migogoro mbalimbali inayowasilishwa kwenye mabaraza hayo.

(Viii) Kamati ilipendekeza Kwamba kila kata ihakikishe inakuwa na mihtasri ya upatikanaji wa Ardhi zinazomilikiwa na taasisi za Serikali zilizopo katika kata husika ili kuepusha migogoro ya Ardhi.

(iX) Kamati ilipendekeza Kwamba kila mheshimiwa Diwani ahakikishe anaihamasisha jamii kushiriki katika kuchangia miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwenye kata yake.

(X) Kamati ilipendekeza kwamba viwango vya tozo ya ushuru wa mazao vipunguzwe ili wafanyabiashara wa mazao waweze kulipa ushuru bila kutorosha na Halmashauri iweze kupata mapato mengi

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kuwa taarifa hii ipokelewe na kuwa kumbukumbu sahihi za Halmashauri.

Naomba kuwasilisha.

Mhe. Thereza J. Lusangija
**Mwenyekiti,**
**Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango.**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

## HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA

Mwenyekiti,
Baraza la Madiwani,
Halmashauri ya Wilaya,
**KWIMBA.**

### TAARIFA YA KAMATI YA UCHUMI, UJENZI NA MAZINGIRA KWA KIPINDI CHA ROBO YA II , OKTOBA - DESEMBA 2021/2022.

Mhe. Mwenyekiti, mbele yako kuna taarifa ya Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira kwa kipindi cha Robo ya **II** , Oktoba - Desemba 2021/2022.

Wajumbe wa Kamati hii ni hawa wafuatao;

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Peter Misalaba | - | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Athanasi Nigo | - | Mjumbe |
| 3. | Mhe. John Sababu | - | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Bukaba Majoge | - | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Anthon Swagi | - | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Wenslaus Mapolu | - | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Leah Joseph | - | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Sostenes Kijika | - | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Philipo Ndalahwa | - | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Elias Galula | - | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Masanja Imaja | - | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Peter Ngasa | - | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Adelah Charles | - | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Mayala Sagini | - | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Khadija Ndonde | - | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Hole Mashauri | - | Mjumbe |

**Mhe, Mwenyekiti.**

Kwa kipindi cha Robo ya II, Oktoba - Desemba 2021/2022. kamati ilitembelea Miradi minne (04) ambayo ni Mradi wa shamba la mkulima wa pamba Nkalalo , Mradi wa ufyatuaji wa matofali Nyambiti, mradi wa ufugaji wa nguruwe na kilimo cha alizeti Kata ya Sumve na mchoro wa Mipango Miji mtaa wa Ilamba Kata ya Ngudu. Kamati ilifanikiwa kufika katika maeneo yote ya miradi kama ilivyopangwa.

Baada ya Kamati kutembelea miradi hiyo walishauri kama ifuatavyo;-

Wajumbe walishauri na kuelekeza kuwa wataalamu wa kilimo watembelee mashamba ya wakulima wakubwa ili kutoa ushauri wa kitaalam katika ulimaji wa kilimo cha kisasa pia walishauri vikundi vilivyopewa mikopo vifuatiliwe virejeshe fedha kwa wakati ili vikundi vingine viweze kukopa na kupewa maelekezo ya utaratibu mpya wa urejeshwaji wa mikopo hiyo, Pia wajumbe walipongeza kwa kazi nzuri zinazofanyika kwenye miradi yote waliyoitembelea.

Aidha, kwa kipindi cha mwezi Oktoba – Desemba 2021/2022, kamati ilipitia shughuli zilizofanywa na Idara zifuatazo;

- Idara ya Ardhi na Maliasili
- Idara ya Kilimo Umwagiliaji na Ushirika
- Idara ya Maendeleo ya jamii
- Idara ya Mifugo na Uvuvi
- Idara ya Ujenzi na Zimamoto
- Kitengo cha Usafi na Mazingira.
- Kitengo cha Nyuki
- Taarifa ya TASAF

- **Idara ya Kilimo na Umwagiliaji na Ushirika.**

**Mhe.Mwenyekiti.**

Katika kipindi cha robo ya II, Oktoba – Desemba, 2021- 2022 Idara imeratibu zoezi la usambazaji wa mbegu za Pamba Vijijini ambapo jumla ya tani 486 zililetwa na kusambazwa vijijini kati ya tani 600 zilizokuwa zimepangwa kuletwa katika Wilaya ya Kwimba, Kuratibu kampeni ya uhamasishaji wa kuongeza tija katika uzalishaji wa zao la pamba Vijijini ambapo jumla ya wakulima 12,750 walifikiwa na kuhamasishwa katika Kata 23 zenye Vijiji 60 chini ya uhamasishaji wa Balozi wa zao la pamba, Uandaaji,

Kusimamia utoaji na usambazaji wa miche ya mikorosho kwa wakulima ikiwa jumla ya miche ya mikorosho 2,500 ilioteshwa na miche 1,500 imesambazwa kwenye Taasisi na watu binafsi, kufuatilia shughuli za ugani Vijijini ambapo huduma za ugani zimeendelea kutolewa katika Vijiji mbalimbali katika Wilaya ya Kwimba,

Pamoja na kufanya tathimini ya hali ya chakula ambapo gunia la mahindi limeendelea kuuzwa kati ya Tsh.70,000-85,000, kilo ya mchele inauzwa kati ya Tsh1,400-1500 na Kufanya ukaguzi kwenye vyama vya Ushirika vya msingi (AMCOS) ikiwa jumla ya vyama 8 vimekaguliwa.

- **Idara ya Mifugo**

**Mhe. Mwenyekiti.**

Kamati ilipitia taarifa za shughuli za Idara ya Mifugo ikiwa ni pamoja na kuthibiti magonjwa ya mifugo kwa kuogesha kwenye majosho 9 ambapo Ng'ombe 5,187, Mbuzi 515, Kondoo 583 waliogeshwa ikiwa ng'ombe mmoja aliogeshwa kwa Tsh.100 na mbuzi/kondoo ameogeshwa kwa Tsh.50 hivyo jumla ya Tsh.573,600 zilipatikana kutokana na uogeshaji, vilevile ng'ombe 40,365, Mbuzi 4,683, Kondoo 2,381 walinyunyiziwa dawa kwa kutumia pampu za mkono.

Kazizingine zilizo fanyika ni kukagua na kupitisha Nyama katika machinjio ambapo Ng'ombe 597, Mbuzi 378, Kondoo 352 na Nguruwe 31 walichinjwa, walikaguliwa na kupitishwa katika machinjio za Ngudu, Hungumalwa, Nyambiti,Sumve, Malya na Maligisu, kufanya usimamizi wa biashara ya mifugo minadani na ukusanyaji wa maduhuri ambapo Ng'ombe 3990,

Mbuzi 2,900 na Kondoo 1,621 walinunuliwa, kufanya ukaguzi wa mazao yatokanayo na uvuvi na kusimamia shughuli za uvuvi katika bwawa la mahiga ambapo jumla ya Tsh.305,000/= zimekusanywa,

Pia kufanya shughuli za matibabu ya mifugo, kusimamia na kuhamasisha zoezi la chanjo ya mifugo ambapo kuanzia tarehe 14/09/2021 hadi tarehe 07/10/2021 zoezi la chanjo lilikamilika kwa kuchanja ng'ombe 34,153 hivyo kufanya jumla ya ng'ombe wote waliochanjwa kufikia 119,198 kwa Kata zote na kushiriki mafunzo ya kufanya maandalizi ya utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo kwa kutumia hereni.

**Idara ya Usafi na Mazingira.**

**Mhe. Mwenyekiti.**
Katika kipindi cha robo ya II , Mwaka 2021/2022 Kamati ilipitia shughuli zilizofanywa na idara ikiwa ni uhifadhi wa mazingira ambapo jumla ya miti 7,000 ilipandwa katika Taasisi mbalimbali, kushirikiana na Idara ya kilimo katika ukuzaji wa michwe ya korosho ambapo jumla ya miche 3,000 ilikuzwa,

Aidha; kufanya ukaguzi wa mazingira kwa kushirikiana na Kitengo cha Afya kinga katika Kituo cha SGR – Nkalalo, kushiriki katika kufanya tathmini ya athari za mazingira katika miradi itakayotekelezwa na TASAF, kushiriki katika shughuli za usimamizi na ufuatiliaji wa shughuli za ujenzi wa madarasa ya UVIKO – 19 na kushiriki katika vikao mbalimbali vya Kisheria.

**Idara ya Ardhi na Maliasili.**

**Mhe, Mwenyekiti.**
Taarifa iliwasilshwa na Kaimu Afisa Ardhi na Maliasili (W) alieleza kuwa katika kipindi cha Robo ya II, mwaka 2021/2022 Kamati ilipitia taarifa ya kazi zilizofanywa na Idara ya Ardhi ikiwa ni pamoja na kuandaa michoro 3, kutoa vibali vya ujenzi 22 kwa waliokidhi vigezo, kufanya ukaguzi wa nyumba 30 kwa ajili ya kudhibiti ujenzi holela.

Usimamizi na ukusanyaji kodi ya Ardhi ambapo jumla ya Sh. 5,770,150 zimekusanywa na kutumwa Wizara ya Ardhi, nyumba na Maendeleo ya makazi ikiwa ni kodi ya pango la Ardhi.

Kutoa Elimu kwa wananchi juu ya umiliki wa ardhi na ulipaji wa kodi ya pango la ardhi, kufuatilia madeni ya pango la Ardhi ambapo jumla ya Ankara 124 zilitumwa kwa wadaiwa sugu, Kufanya uthamini wa mali na kwa ajili ya kulipa fidia.

**Maliasili.**
**Mhe, Mwenyekiti.**
Shughuli nyingine ni Usimamizi wa Maliasili ambapo kiasi cha tsh 350,000 zlikusanywa ikiwa ni mapato yatokanayo na mazao ya misitu, Utunzaji na uanzishaji wa vitalu vya misitu ambapo jumla ya miche 30,374 iliotesha katika vitalu/bustani,

Pia kushirikiana na Wakala wa huduma za misitu (TFS) kupokea miti 25,813 kutoka katika vitalu vilivyokuzwa na TFS na kusambazwa sehemu mbalimbali, kushiriki katika zoezi la kupambana na wanyamapori wakali dhidi ya wananchi na kushiriki katika vikao mbalimbali vya Kisheria.

- **Kitengo cha nyuki;**

**Mhe, Mwenyekiti.**
Kamati ilipitia taarifa za Kitengo cha Nyuki kwa kipindi cha robo ya II, mwaka 2021/2022 ni kutoa elimu ya ufugaji Nyuki wenye tija pamoja kusimamia uzalishaji na uvunaji wa Asali ambapo jumla ya kilo za Asali 100 zilivunwa na zimeuzwa kwa Sh. 10,000/= kwa lita, kufanya ukaguzi wa mizinga 38 na kubaini mizinga 12 haina nyuki kati ya 59, kuandaa taarifa mbalimbali na kushiriki katika vikao mbalimbali.

- **Idara ya Maendeleo ya Jamii;**

**Mhe, Mwenyekiti.**
Katika kipindi cha robo ya II, Kamati ilipitia taarifa ya shughuli zilizofanywa na Idara ikiwa ni kufuatilia marejesho ya mikopo ambapo jumla ya Sh.50,231,850 zimerejeshwa kutoka kwenye vikundi 105, kutoa mikopo ya asilimia 10 kutoka kwenye mapato ya ndani ambapo jumla ya Sh.50,177,955.33 zilitolewa, kutoa mikopo iliyotokana na fedha za marejesho kiasi cha Sh.90,911,883.83 kwa vikundi 22,

Aidha, shughuli nyingine ni kuratibu na kusajili mashirika yasiyo ya Kiserikali ambapo jumla ya vikundi 29 vilisajiliwa na walichangia jumla Tsh 290,000/= kama gharama ya usajili, kuratibu maendeleo ya jinsia ambapo watu 339 walipewa elimu juu ya masualaya ukatili chini ya mdau KWIPAU, kuratibu masuala mtambuka ya UKIMWI, LISHE,CHF n.k ambapo jumla ya watu 69 walishiriki wakiwemo viongozi 13, kusambaza Kondomu 1300 kwa wamachinga wadogo wadogo,

Vilevile; kusambaza Kondomu 49,206 kwenye Kata mbalimbali, kuhamasisha umuhimu wa lishe bora kwa wamama wajawazito na wenye watoto wachanga kuanzia umri wa miezi 6 ambapo jumla ya kina mama 40 walishiriki na kufanya uhamasishaji wa wananchi kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) ambapo jumla ya kaya 308 zimejiunga na kadi 9000 zimepokelewa kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na kushiriki katika shughuli mbalimbali za mradi wa TASAF.

**Kitengo cha TASAF;**

**Mhe, Mwenyekiti.**
Kamati ilipitia shughuli lilizofanywa na Kitengo cha TASAF ikiwa ni pamoja na kusimamia malipo katika Vijiji 86 kwa walengwa wa TASAF III ambapo jumla ya Kaya 7,751 kati ya 7880 zililipwa kiasi cha Sh.360,842,000 /= kati ya Sh.368,392 zilizolengwa ikiwa ni sawa na 98.36%, kutoa taarifa mbalimbali za shughuli za TASAF,

Vilevile kushughulikia malalamiko mbalimbali ya walengwa wa TASAF, kuandaa vikundi vya walengwa vya kuweka na kuwekeza katika vijiji hivyo 86 ambapo jumla ya vikundi 527 viliundwa, kuandikisha walengwa wa mpango katika mfumo wa kielektroniki ambapo jumla ya

Kaya 1,099 kati ya 7,880 walisajilia katika mfumo na kushiriki katika vikao mbalimbali vya Kisheria.

**Idara ya Ujenzi:**

**Mhe, Mwenyekiti.**

Kamati ilipitia taarifa za kazi zilizotekelezwa na Idara ya ujenzi ikiwa ni usimamizi wa ujenzi wa Majengo 12 ambayo ni Jengo la OPD na jengo la Maabara Jengo la Utawala, Jengo la Mionzi, Jengo la kuhifadhia ya Dawa, Jengo la kuhifadhia Maiti Nyumba 3 za watumishi na Wodi ya wanawake na wanaume katika Hospitali ya Wilaya eneo la Icheja,
Kusimamia ujenzi wa kituo cha Afya Kadashi, kwa majengo ya Maabara na wodi ya wazazi

Aidha; kusimamia Miradi ya EP4R katika Shule za msingi na Sekondari ambapo kulikuwa na ujenzi wa madarasa na matundu ya vyoo kazi zimekamilika.Kusimamia na kufuatilia ujenzi wa madarasa 109 ya mradi wa mapambano dhidi ya UVIKO -19

Usimamizi na ufuatiliji wa Ujenzi wa Bweni Shule ya Sekondari Bupamwa na Tallo kazi zinaendelea pamoja na kuandaa makadirio ya vifaa vya ujenzi katika miradi ya Afya, Elimu Msingi na Sekondari

Aidha; kamati ilipitia taarifa za miradi ya maendeleo kwa kipindi cha Robo II 2021/2022 Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba iliidhinishiwa kukusanya, kupokea na kutumia Sh. 15,476,782,310.00 kutoka Serikali Kuu na wadau wa maendeleo ikiwa ni ruzuku kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Disemba 2021. Halmashauri imepokea Sh. 11,285,524,371.32 sawa na 72.92% ya lengo kuu la mwaka wa fedha 2021/2022.

**Miradi ya maendeleo kutokana na fedha za mapato ya ndani.**

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022, Halmashauri ilikasimia kukusanya na kutumia Sh. 650,736,400.00 ambayo ni 40% ya makisio ya mapato ya ndani ya Halmashauri kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ambapo kuanzia Julai hadi Disemba 2021, jumla ya Sh. 339,886,407.42 sawa na 52.23% ya lengo kuu la mwaka zilitolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo mbalimbali.

Baada ya kupitiataarifa hizo Wajumbe walitoa mapendekezo yafuatayo.

**Mapendekezo ya Kamati ya Uchumi**

- Kamati ilipendekeza kuwa kila Taasisi za Umma wapande miti katika maeneo yao.
- Kamati ilipendekeza kuwa elimu itolewe kwa wananchi na wamiliki wa nyumba za kulala wageni ili wadhibiti maji machafu tiririka kwa kuchimba shimo la maji machafu kuingia humo.
- Wajumbe wa kamati walipendekeza kwamba kitengo cha Nyuki kinunuliwe vifaa kwa ajili ya shughuli za urinaji/ uvunaji wa asali.
- Wajumbe wa kamati walipendekeza kwamba kila Kamati wasomewe majukumu yao ili kuepusha mgongano na mwingiliano wa majukumu.

- Wajumbe wa kamati walielekeza kuwa Idara ya Ardhi ifuatilie TARURA ili kujua barabara za maeneo yaliyopimwa ya Ngudulugulu na Hungumalwa yachongwe.
- Wajumbe wa kamati walipenda wapewe taarifa ya idadi ya Vikundi vilivyo sajiliwa, vilivyopewa mikopo na vilivyo fikia hatua nzuri za kujikwamua kiuchumi .
- Kamati ilipendekeza kuwa uandaliwe mpango mkakati wa kukusanya mapato yatokanayo na uvuvi wa samaki katika Bwawa la Mahiga .

- Wajumbe wa kamati walipendekeza kuwa uandaliwe Mpango mkakati wa ukusanyaji wa mapato ya Minada kabla ya kuweka uzio.
- Wajumbe wa kamati walipendekeza kwamba Idara ya Ardhi na Maliasili iwasilishe orodha ya Taasisi ambazo zimepimwa maeneo yake na ambazo bado hazijapimwa.

Mhe; Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kuwa taarifa hii ipokelewe na kuwa kumbukumbu sahihi ya Halmashauri,

Naomba kuwasilisha.

Mhe. Peter Misalaba Nyanda,
**Mwenyekiti,**
**KAMATI YA UCHUMI, UJENZI NA MAZINGIRA.**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

## HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA

Mhe. Mwenyekiti,
Baraza la Madiwani,
Halmashauri ya Wilaya,
**KWIMBA.**

**YAH: TAARIFA YA KAMATI YA ELIMU NA AFYA KWA ROBO YA II, OKTOBA – DESEMBA MWAKA 2021/2022.**

Mhe. Mwenyekiti,

Mbele yako kuna taarifa ya kamati ya Elimu na Afya kwa kipindi cha Robo ya **II, Oktoba – Desemba mwaka 2021/2022** Kamati hii ina jumla ya Wajumbe 17 ambao waliteuliwa kwenye mkutano wa Baraza la tarehe 02/12/2020/2021, orodha ya wajumbe hao ni kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Elias Kapunda - Mwenyekiti
2. Mhe. Bukombe Nyanda - Mjumbe
3. Mhe. Yohana N. Shine - Mjumbe
4. Mhe. Teddy Alphonce - Mjumbe
5. Mhe. Joseph Katuli - Mjumbe
6. Mhe. Chenyenge John - Mjumbe
7. Mhe. Tabu M. Ndododo - Mjumbe
8. Mhe. Malando Sanduli - Mjumbe
9. Mhe. Devotha S. Manane - Mjumbe
10. Mhe. Samson Masalu - Mjumbe
11. Mhe. Bayega Nchimanchalo - Mjumbe
12. Mhe. Sephania Cheyo - Mjumbe
13. Mhe. Veronika Manyongo - Mjumbe
14. Mhe. Gervas Kitwala - Mjumbe
15. Mhe. Winfrida Mahumbi - Mjumbe
16. Mhe Majaliwa Mbassa - Mjumbe
17. Mhe. . Thereza J. Lusangija - Mjumbe

Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kipindi cha Robo ya II, Oktoba - Desemba 2021/2022 Kamati ya Elimu na Afya ilifanya Ziara ya kutembelea miradi 4 ambayo ni Ukaguzi wa miundombinu katika shule ya msingi Bushini, Kukagua miundombinu katika Shule ya Msingi Kabale, kutembelea, kukagua na kuona hali ya Utoaji wa huduma katika kituo cha Afya Mwamashimba Pamoja na

ukaguzi wa hali ya Miundombinu ya vyumba vya madarasa 7 katika Sekondari ya Hungumalwa

. Kamati ilifanikiwa kufika katika maeneo yote ya miradi kama ilivyopangwa.

Aidha, kwa kipindi cha mwezi Oktoba – Desemba 2021/2022, kamati ilipitia shughuli zilizofanywa na Idara zifuatazo;

- Idara ya Elimu Msingi.
- Idara ya Elimu Sekondari.
- Idara ya Afya.
- Miradi ya TASAF

**Idara ya Elimu Msingi**

Katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2021/2022 Shughuli zilizofanyika katika Idara ya Elimu Msingi ni Kufanya sensa ya maotea ya watoto watakaoandikshwa darasala awali ,darasa la kwanza na wanafunzi wenye mahitaji maalum, ambapo jumla ya watoto 13,327 wataandikishwa madarasa ya awali na watoto 13,854 waliandikishwa darasa la kwanza mwaka 2021, kuratibu na kusimamia uendeshaji wa Mtihani wa Taifa wa darasa la nne (SFNA) Mwaka 2021 ambapo jumla ya watahiniwa 13,266 walifanya mtihani sawa na asilimia 93.5,

Kufanya uhakiki wa usajili wa wanafunzi watahiniwa wa PSLE, kufanya ufuatiliaji na kuratibu zoezi la ufundishaji na ujifunzaji kwenye shule, kuratibu na kusimamia ujenzi wa miradi ya EP4R na samani mbalimbali, kufanya maandalizi ya mtihani wa SFNA 2021, kuratibu uendeshaji wa mafunzo ya kudhibiti ubora wa ndani ya shule na kufanya maandalizi ya kikao cha wadau wa Elimu ambapo jumla ya walimu wakuu 77 walishiriki ,

Kupokea na kugawa vitabu 325 vya mwongozo, kufuatilia na kuhimiza maendeleo ya taaluma katika klasta zote, Kuchambua na kuandaa orodha ya waalimu wanaostahili kwenda likizo ambapo jumla ya waalimu 262 walienda likizo mwezi Desemba 2021 na kulipwa jumla ya Tsh 53,525,000.00
Kuratibu maandalizi na kufanya ufuatiliaji wa zoezi la ufanyikaji mtihani wa darasa la VII PSLE uliofanyika nchini kote Oktoba, 2021 na kushiriki katika kuchagua wafunzi wa kidato cha kwanza mwaka 2022.

**Idara ya Elimu Sekondari**

Katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2021/2022 Shughuli zilizofanyika katika Idara ya elimu Sekondari ni; kufuatilia hali ya ufundishaji Shuleni ambapo hali ya ufundishaji ni asilimia 86. kufungua muhula wa pili (02) wa masomo kwa kipindi cha mwaka 2021, kushiriki kwenye zoezi la usimamizi na uendeshaji wa mtihani kidato cha IV na kidato cha II mwaka 2021 ambapo jumla ya wanafunzi 4,447 walifanya mtihani wa kidato cha pili sawa na asilimia 89 kati ya 4,983,

Kushughulikia ufuatiliaji na usimamizi wa ujenzi wa vyumba vya madarasa 109 ya mradi wa mapambano dhidi ya UVIKO-19 ambapo kiasi cha fedha Tsh 2,180,000,000.00 zililetwa, kushiriki katika kuchagua wafunzi wa kidato cha kwanza mwaka 2022.

kufanya semina kwa walimu wote 355 wanaofundisha madarasa ya mitihani kusimamia ujenzi wa miundombinu mradi wa EP4R katika Shule, Kushughulikia likizo za walimu kwa Desemba, 2021 ambapo walimu 128 walilipwa kiasi cha jumla Tsh.30,278,000/= za likizo, Kushiriki katika Uchaguzi wa wanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka 2022.

Aidha, Kupokea Tsh 532,500,000.00 za kukamilsha madarasa na maabara ambapo ukamilishaji wa maabara 8 za sekondari zimepelekewa jumla ya tsh 232,500,000,000, kiasi cha 225,000,000.00 za ukamilishaji wa vyumba 18 vya madarasa na kiasi cha Tsh75,000,000.00 za ukamilishaji wa vyumba vya madarasa kwa shule 3 , Kufanya tathimini ya ya mapokezi ya wanafunzi wa kidato cha kwanza 2022 kwa kuwapa maelekezo walimu wakuu.

Pamoja na Kufanya ufuatiliaji wa upungufu wa miundombinu kwa shule zote 34 ambapo upungufu wa vyumba vya madarasa, meza na viti pia kufanya mapokezi ya fedha za elimu bila malipo ambapo jumla ya Tsh 228,460,435.35 zilipokelewa.

**Idara ya Afya**

Katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2021/2022 Shughuli zilizofanyika ni kuongeza uwepo wa wataalamu wa Afya katika vituo vya kutolea huduma kutoka 38%-50% kufikia Juni 2022 ambapo watumishi 10 wameajiria kwa mkataba chini ya AMREF, kutoa huduma ya kitabibu kwa wagonjwa, kufanya uhamasishaji wa usafi wa mazingira ikiwemo uhamasishaji wa ujenzi wa vyoo bora ngazi ya kaya kutoka 25%- 30% kufikia Juni 2022, kuongeza kiwango cha uzazi wa mpango kutoka 47% hadi 37% ifikapo Juni 2022, kupunguza vifo vya akina mama kutoka 78/100,000 hadi 74/1000,000 kufikia Juni 2022, kupunguza idadi ya vifo vya watoto chini ya miaka 5 kutoka kifo1 /1000 – 0.5/1000 fikapo Juni,2022.

Vilevile Kupunguza maambukizi ya Malaria kutoka 22.4% -20% ifikapo Juni,2022 kupunguza maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto kutoka 2% -1.3% ifikapo Juni 2022, Kuongeza ukusanyaji wa damu salama kutoka 60%-90% kufikia juni 2022,Kutoa chanjo mbalimbali ambapo watoto 6,123 wenye umri wa chini ya miaka 5 walipapewa chanjo sawa na 92.6% wajawazito 3,242 walipewa chanjo na jumla ya watu wazima 8,866 walipewa chanjo ya UVIKO-19 ambapo chanjo aina ya Pfizer watu 4,627 na awamu ya pili chanjo ya Sinopharm watu 4,239 walichanjwa.

Aidha, kuongeza utambuzi wa wagonjwa wa TB kutoka 2% -6.2% kufikia Juni 2022, Kuimarisha huduma za lishe kwenye Wilaya, kupunguza uhaba wa madawa, vifaa tiba na vitenganishi kutoka 47% -20 % ifikapo Juni,2022 ambao kwa sasa upo kwa 16% ,Vilevile kuongeza idadi ya wanachama wa mfuko wa Afya ya Jamii ICHF kutoka 3% - 5% ifikapo Juni,2022 ambapo jumla ya kaya

174 zimejiunga na jumla ya Tsh 5,220,000 zimekusanywa, kupunguza maambukizi ya UKIMWI kutoka 4.8% hadi 3.5% kufikia juni 2022.

**MIRADI ITAKAYOTEKELEZWA NA TASAF MWAKA 2022**

Kamati ilipitia taarifa ya miradi itakayotekelezwa na TASAF (W) katika sekta mbalimbali ndani ya Halmashauri

Kwa sekta ya Elimu Msingi na Elimu Sekondari vipaumbele vinavyozingatiwa ni ujenzi wa miundombinu ya elimu kama vile vyumba vya madarasa, nyumba za walimu, matundu ya vyoo, Ofisi za walimu, maabara na mabweni.

Kwa sekta ya Afya vipaumbele vinavyozingatiwa ni ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya kutolea huduma za Afya kama vile wodi za wagonjwa, Hospitali, Vituo vya Afya, Zahanati na nyumba za watumishi Sekta ya Mifugo na Uvuvi vipaumbele vinavyozingatiwa ni miundombinu ya mifugo malambo, majosho,vibanio, mabirika ya kunyweshea maji, vifaa vya kutolea huduma kama majokofu

aliwasilisha orodha ya miradi inayopendekezwa kisekta kama ifuatavyo;

**ORODHA YA MIRADI INAYOPENDEKEZWA KISEKTA**
**ELIMU MSINGI**

| NA. | JIMBO | KATA | KIJIJI | MIRADI PENDEKEZWA | MAKISIO YA BAJETI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | KWIMBA | NG'HUNDI | Igunguhya | Ujenzi wa madarasa 3 na matundu 6 ya vyoo katika shule ya msingi Kabale. | 88,400,738.6 |
| 2 | KWIMBA | SHILEMBO | Nghuliku | Ujenzi wa madarasa 3 na matundu 6 ya vyoo katika shule ya msingi Nghuliku. | 89,980,284.0 |
| 3 | KWIMBA | HUNGUMALWA | Buyogo | Ujenzi wa madarasa 3 na matundu 6 ya vyoo katika shule ya Msingi Mwamaya. | 88,275,738.6 |
| 4 | KWIMBA | KIKUBIJI | Mwamitinje | Ujenzi wa madarasa 3 na matundu 6 ya vyoo katika shule ya Msingi Mwamitinje. | 89,882,784.0 |

**ELIMU SEKONDARI**

| NA. | JIMBO | KATA | KIJIJI | MIRADI PENDEKEZWA | MAKISIO YA BAJETI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | KWIMBA | SHILEMBO | Shilembo | Ujenzi wa nyumba za walimu(2 in 1) shule ya sekondari Shilembo. | 67,006,250.00 |

**AFYA**

| NA. | JIMBO | KATA | KIJIJI | MIRADI PENDEKEZWA | MAKISIO YA BAJETI |
|---|---|---|---|---|---|

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | KWIMBA | NGUDU | Ngudu mjini | Ujenzi wa zahanati kijiji cha Kilyaboya.(Awamu ya I)<br><br>Umaliziaji wa zahanati kijiji cha Kilyaboya.(Awamu ya II) | 70,294,318.1<br><br>89,632,386.3 |
| 2 | SUMVE | MALYA | Mwitambu | Ujenzi wa nyumba ya mtumishi (2 in 1) zahanati ya Mwitambu. | 67,006,250.0 |
| 3 | SUMVE | SUMVE | Nyamikoma | Ujenzi wa zahanati kijiji cha Nyamikoma.(Awamu ya I)<br><br>Ukamilishaji wa zahanati kijiji cha Nyamikoma.(Awamu ya II) | 70,294,318.1<br><br>89,632,386.3 |

**ORODHA YA MIRADI YA KUTOA AJIRA KWA MUDA ( PWP)**

| NA. | JIMBO | KATA | KIJIJI | MIRADI PENDEKEZWA | MAKISIO YA BAJETI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | SUMVE | MALIGISU | Kadashi | Ujenzi wa Lambo kijiji cha Kadashi. | 75,010,340.91 |
| 2 | SUMVE | NYAMBITI | Nyambiti. | Ujenzi wa Lambo kijiji cha Nyambiti. | 75,004,090.91 |
| 3. | KWIMBA | FUKALO | Sanga | Ujenzi wa barabara za vitongoji vya Isunda kwenda Sima A na Sima B. | 75,162,436.36 |

**ORODHA YA MIRADI YA VIKUNDI (INCOME GENERATING ACTIVITY) IGA**

| NA. | JIMBO | KATA | KIJIJI | MIRADI PENDEKEZWA | MAKISIO YA BAJETI(Tshs) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | KWIMBA | NYAMILAMA | Nyamilama | Ufugaji wa mbuzi katika vikundi 5 vya walengwa kijiji cha Nyamilama. | **25,220,454.00** |
| 2 | SUMVE | MALYA | Mwamhembo | Ufugaji wa mbuzi na kondoo katika vikundi 5 vya walengwa kijiji cha Malya. | **23,819,659.00** |

Baada yawajumbe kufanya Ziara na tathimini yake pamoja na kupitia taarifa za Idara,**na miradi ya TASAF Wajumbe walitoa mapendekezo yao ;**
**Kamati ilipendekeza kama ifuatavyo:**

- Kamati ilipendekeza Serikali ya Kijiji, Jamii na wadau mbalimbali washirikishwe katika kukamilisha miundombinu ya Shule ya Msingi Bushini ikiwa ni kukarabati vyumba vya madarasa kwa kupaka rangi na kuweka sakafu, utengenezaji wa madawati,kuweka utaratibu wa kuwasaidia wanafunzi kuvuka barabarani ili kuepusha ajali. Pamoja na kuchimba mtaro ili kuzuia maji machafu kuingia katika eneo la shule na kuweza kusababisha milipuko ya magonjwa kwa wanafunzi

- Kamati ilipendekeza kwamba Shule ya msingi Kabale ipewe kipaumbele cha kupewa fedha kutoka katika vyanzo mbalimbali pindi inapotokea fulsa ili kuboresha miundombinu ya shule msingi Kabale

- Kamati ilipendekeza Jamii ishirikishwe katika kukamilisha miundombinu ya Shule ya Msingi Kabale.ikiwa ni pamoja na ukamilishaji wa matundu ya vyoo, vyumba vya madarasa,ili wanafunzi waweze kusoma katika mazingira bora

  Kamati ilipendekeza Shule ya Sekondari Hungumalwa itengeneze viwanja vya michezo ili kukuza vipaji vya watoto. Halmashauri iendelee kutenga fedha kwaajili ya kuongeza miundombinu ya shule ya sekondari Hungumalwa

- Kamati ilipendekeza ufuatiliaji ufanyike kwa kuwashirikisha Wabunge ili Vituo vya Afya viweze kupatiwa vifaa tiba. Pia walisema yanapoanzishwa majengo ya kutolea huduma za Afya yawekwe makadirio/bajeti ya kuweka uzio.

- Kamati ilipendekeza Kituo cha Afya Mwamashimba kipatiwe jenereta lenye nguvu zaidi litakalosaidia wakati wa upasuaji (operation) na kuhifadhi damu pindi umeme unapokatika

- Kamati ilipendekeza jengo la kuhifadhia maiti katika Kituo cha Afya Mwamashimba liwekewe umeme na majokofu

- Kamati ilipendekeza Kituo cha Afya Mwamashimba kijengewe stendi ya kuweka tenki la kuhifadhia maji

- Kamati ilipendekeza kuwa fedha za ukamilishaji na ujenzi wa miradi ya Vituo vya kutolea huduma za Afya na Elimu zitumike haraka kwa kufuata taratibu kabla ya muda wake kuisha ili zikamilishe miradi hiyo kwa muda uliokusudiwa.

- Kamati ilipendekeza eneo la kujenga Kituo cha Afya Hungumalwa lipatikane mapema ili ujenzi uweze kuanza haraka.

- Kamati ilipendkeza kwamba Jamii ihamasishwe kikamilifu kushiriki katika utekelezaji wa miradi ya TASAF

Mhe. Mwenyekiti naomba kutoa hoja kuwa taarifa hii ipokelewe na kuwa kumbukumbu sahihi za Halmashauri.

Naomba kuwasilisha.

Mhe. Elias Kapunda

**MWENYEKITI, KAMATI YA ELIMU NA AFYA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA**

Mhe. Mwenyekiti,
Baraza la Madiwani,
Halmashauri ya Wilaya,
**KWIMBA.**

**YAH: TAARIFA YA KAMATI SHIRIKISHI YA KUDHIBITI UKIMWI KWA KIPINDI CHA ROBO YA II OKTOBA - DISEMBA, 2021/2022**

Mhe. Mwenyekiti,

Mbele yako ni taarifa ya Kamati Shirikishi ya kudhibiti UKIMWI kwa kipindi cha robo ya II, Oktoba - Desemba, 2021/2022.

Kamati hii ina jumla ya wajumbe sita (6) waliteuliwa kwenye Mkutano wa Baraza la Madiwani la tarehe 02/12/2020.

Orodha ya Wajumbe wa kamati ni kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Lucy Nchangwe - Mwenyekiti
2. Mhe. Khadija Ndode - Mjumbe
3. Mhe. John Sababu - Mjumbe
4. Mhe. Leah Joseph - Mjumbe
5. Mhe. Mapembe T. Ndododo - Mjumbe
6. Mhe. Mayala Sagini - Mjumbe

Aidha, kwa kipindi cha Oktoba - Desemba, 2021/2022. Kamati ilipitia taarifa za shughuli za mapambano dhidi ya UKIMWI.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha robo ya Pili 2021/2022 shuguli zilizofanyika ni kutoa Elimu ya Mapambano dhidi ya UKIMWI kwa kushirikiana na mdau shirika la CSSSC ( CHRISTIAN SOCIAL SERVICES COMMISION ), kuandika katiba kwa WAVIU ambapo wanawake vinara 12 na wazee maarufu 6 walishiriki.
Kushiriki katika maazimisho ya siku ya UKIMWI Duniani iliyofanyika katika kijiji cha Mhalo katika kata ya Bupamwa ambapo elimu ya umuhimu wa mapambano dhidi ya UKIMWI ilitolewa kwa watu 511 na viongozi 13 walishiriki. Kutoa elimu ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya UKUMWI na matumizi sahihi ya Kondom kwa wachimbaji wadogo wadogo 56 wa madini katika machimbo ya Kiliwi na Mhalo.

Kutoa elimu ya kujikinga na maambukizi dhidi ya UKIMWI kwa viongozi wa vikundi 43 vya wajasiliamali.Pamoja na kushirikiana na wadau wawili wa mapambano dhidi ya UKIMWI ambao ni CSSC na ICAP.

Mheshimiwa Mwenyekiti kamati yako ilipitia taarifa ya utoajiwa elimu kwa vijana wenye umri wa miaka 10-24 ambapo jumla ya vijana 56 walishiriki.

Kutoa elimu ya matumizi sahihi ya Kondom za kiume kwa vijana 76 wenye umri wa miaka zaidi ya 25 .

Kutoa elimu ya matumizi sahihi ya kondomu kwa wafanyakazi 56 wa migodini.

Kusambaza pisi 49936 za kondomu kwenye kata mbalimbali ndani ya wilaya ya Kwimba.

Kushiriki katika kutoa huduma za kukabiliana na athari za VVU kwa Yatima wanaishi katika mazingira hatarishi, makundi ya watu wanaishi na VVU na wazee.

Mhe mwenyekiti kamati yako ilipitia taarifa ya Ufuatiliaji wa makundi saba ya watu wanayoishi na Virusi vya UKIMWI. Kutoa mafunzo katika kujenga uwezo kuhusu kujikinga na VVU na UKIMWI, usimamizi wa huduma, mafunzo na matibabu pamoja na kukabiliana na athari za VVU.

**Huduma za UKIMWI na VVU zilizotolewa na Idara ya Afya;**

Mhe. Mwenyekiti Kamati pia ilipitia taarifa za kazi zilizofanywa na Idara ya Afya ambapo wateja waliopima VVU na kupokea majibu yao walikuwa Me 4,724 na Ke 6,198.

Waliopimwa wakapatikana na VVU ni Me 144 na Ke 369. Walioanzishiwa dawa za kufubaza makali ya VVU Me 103 na KE 204. Wajawazito walio hudhuria Kliniki na kupimwa walikuwa 3,525 na walio gundulika kuwa na VVU Ke 67, wajawazito walioanza dawa ni 67.

Idadi ya watoto waliozaliwa na wanawake wanaoishi na VVU ME 29 na Ke 36, idadi ya watoto walioandikishwa na kuanzishiwa NVP Syrup baada ya kuzaliwa Me 23 na Ke 28.

Jumla ya watoto walioanzishiwa dawa ya contimoxazole Me 23, Ke 28

Watoto waliopimwa VVU kwa kipimo cha kwanza DNA PCR Me 23 na Ke 27. Waliothibitika kuwa na VVU kwa kipimo cha pili Me 0 na Ke 1.

Idadi ya watu wanaoishi na VVU waliopimwa na kuthibitika kuwa na TB Me 6, Ke 4.

Idadi ya watu wanaoishi na VVU waliothibitika kuwa na TB waliotibiwa na kumaliza tiba Me 2, Ke 3.

Watoto walioandikishwa katika Vituo vya matibabu ya CTC ME 0 na Ke 0, idadi ya watoto waliopimwa kuwa na TB Me 0 na Ke 0.

Kufanya tathmini ya VVU na UKIMWI kuhusu ushiriki wa wanandoa katika Zahanati sita ambazo ni Zahanati ya Ibindo, Shushi, Mwakilyambiti Shilembo, Nyambui na Kiliwi.

Kutoa elimu kwa kina baba 43 kuhusu umuhimu wa kina baba kwenda kupima Afya zao na wenzi wao katika Zahanati 6 za Vijiji vya Ibindo, Shushi, Mwakilyambiti, Shilembo, Nyambui na Kiliwi.

Kufanya ufuatiliaji wa shughuli zinazofanywa na Mdau TIP za upimaji UKIMWI katika CTC tano ambazo ni Sumve, Buyogo, Mwangika, Mwamashimba na Bungulwa

Kufanya ufuatiliaji wa mradi wa kuwatengenezea watoto wa kiume kuwa wanaume bora katika Shule ya Msingi Jojiro ambapo watoto 70 waliingizwa

Kutoa elimu ya matumizi sahihi ya Kondomu kwa waganga 2 na Layconcelor 7 wa Vituo vya kutolea huduma za Afya 2 vya Buyogo na Mwamashimba.

Kubaini mahitaji ya kondomu za kiume katika Kata 30 za Wilaya ya Kwimba. Pamoja na kutoa elimu ya maambukizi mapya ya Ukimwi na matumizi sahihi ya kondomu kwa wamiliki wa baa na nyumba za kulala wageni katika Kata ya Ngudu.

Taarifa ya utekelezaji wa Afua za Ukimwi kwa robo ya I Julai – Septemba, 2021-2022

**Huduma za Kinga.**

Katika kipindi cha robo ya II, Oktoba -Desemba, 2021/2022 wanajamii waliofundishwa elimu ya ujasiliamali na stadi za maisha ni 56 kutoka katika Tarafa ya Ngudu, Ngulla, Nyamilama, Mwamashimba na Ibindo

Vijana wenye umri zaidi ya miaka 25 waliopata elimu ya matumizi sahihi ya Kondomu 102, kati yao Me 74, Ke 28 kutoka katika Tarafa zote 4.

Waliopata elimu ya Ujasiliamali ni 273 Me ni 248 na Ke ni 25 kutoka Tarafa ya Ngudu, Ibindo, Ngula na Nyamilama na waliopata msaada wa Kisaikolojia ni 105 kati yao Me ni 28 na Ke ni 77 kutoka Tarafa ya Ngudu, Nyamilama, Ngulla, Ibindo na Mwamashimba, waliopata elimu ya mila na desturi 105, Me ni 28 na Ke ni 77 Tarafa ya Mwamashimba na Ibindo.

Mhe. Mwenyekiti Kamati ilitoa mapendekezo yafuatayo;

- Kamati ilipendekeza kwamba elimu iendelee kutolewa kwa jamii kuhusu kupima Afya zao na kujitambua,

- Kamati ilipendekeza kwamba Kondomu zisambazwe kwa kila Kata ili jamii iweze kupata huduma karibu zaidi na mazingira yao ili kupunguza maambukizi ya VVU

- Kamati ilipendekeza kuwa mdau wa mapambano dhidi ya UKIMWI anapounda makundi ya kufanyanao kazi katika jamii ashirikishe wazee maarufu

- Kamati ilipendekeza Jamii ihamasishwe ili wajawazito na wenzi wao wahudhurie kliniki na kupima UKIMWI.

- Kamati ilipendekeza kuwa Kitengo cha Ustawi wa Jamii wanapopeleka misaada katika Jamii wawashirikishe Waheshimiwa Madiwani

Mhe. Mwenyekiti natoa hoja kuwa taarifa hii ipokelewe na kuwa kumbukumbu sahihi za Halmashauri.

Naomba kutoa hoja kuwa taarifa hii ipokelewe na kuwa kumbukumbu sahihi za Halmashauri

Lucy S. Nchangwe,

**MWENYEKITI KAMATI SHIRIKISHI YA KUDHIBITI UKIMWI.**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

## HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA

Mwenyekiti,
Baraza la Madiwani,
Halmashauri ya Wilaya,
**KWIMBA.**

**YAH: TAARIFA YA KAMATI YA MAADILI KWA KIPINDI CHA ROBO YA II, OKTOBA –DESEMBA MWAKA 2021/2022.**

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha taarifa ya kamati ya maadili kwa kipindi cha robo ya pili kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mhe. Mwenyekiti kamati hii ya maadili ina jumla ya wajumbe watano (5) ambao waliteuliwa kwenye mkutano wa Baraza lilofanyika tarehe 02/12/2020, wajumbe hao ni:-

**KAMATI YA MAADILI**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | Mhe. Athanas Nigo | - | Mwenyekiti |
| 2 | Mhe. Elias Galula | - | Mjumbe |
| 3 | Mhe. Teddy Alphonce | - | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Gervas Kitwala | - | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Philipo Ndalah'wa | - | Mjumbe |

Mhe. Mwenyekiti katika kipindi cha robo ya II, kuanzia Oktoba - Disemba mwaka 2021/2022 kamati ilikaa, kupitia mwongozo wa Kanuni za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) (Maadili ya Madiwani) za Mwaka 2000 kuhusu maadili kwa Wah. Madiwani.Juu ya uvunjaji wa maadili na utekelezaji wa adhabu

Mhe Mwenyekiti Baadhi ya makosa ya kimaadili ni

Kumzuia au kukataza kutekeleza maelekezo yaliyotolewa au kumkwamisha mtumishi wa Halmashauri au kamati kufanya shughuli iliyopangwa, kushindwa kuepuka kufanya jambo lolote linalokatazwa kimaadili, vilevile iwapo atashindwa au atazembea kutekeleza taarifa ua maelekezo yaliyotolewa .

Aidha.kamati ilipewa ufafanuzi kuwa lalamiko la uvunjaji wa kanuni za maadili huweza kutolewa na:- Mtu yeyote ambaye ameathiriwa au anaelekea kuathiriwa na kitendo au maamuzi yaliyofanywa na diwani, mtumishi wa Halmashauri anaweza kutoa lalamiko, diwani anaweza kutoa lalamiko,

Vilevile kamati ya maadili inaweza kutoa lalamiko pia lalamiko hilo hutolewa kwa kujaza fomu maalum kutoka kwa katibu wa kamati ya maadili ambaye ni Afisa utumishi na utawala Wilaya.

Baada ya shughuli hizo, Kamati ilitoa mapendekezo yafuatayo;

- Kamati ilipendekeza kwamba Waheshimiwa Madiwani wasome kanuni za Maadili zote na kanuni za kudumu za Halmashauri.

- Kamati ilipendekeza kuwa usimamizi wa kanuni za vikao uzingatiwe muda wa uchangiaji Hoja dakika tano (05).

- Kamati ilipendekeza kuwa Kila Diwani azingatie utunzaji wa siri za Vikao na Watumishi wanaoingia kwenye vikao hivyo.

- Kamati ilipendekeza wajumbe walipendekeza kuwa katika vikao itumike lugha ya staha na heshima ili kuepusha kukwaza wajumbe wengineMhe. Mwenyekiti, natoa hoja kuwa taarifa hii ipokelewe na kuwa kumbukumbu sahihi za Halmashauri.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kuwa taarifa hii ipokelewe na kuwa kumbukumbu sahihi za Halmashauri.

Naomba kuwasilisha.

Mhe. Athanas Mayunga Nigo
**Mwenyekiti, Kamati ya Maadili**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA.**